Al-Islam.org
Ahlul Bayt Digital Islamic Library Project
Published on *Al-Islam.org* (https://www.al-islam.org)

Nahjul Balaghah – Juzuu ya Kwanza

Publisher(s):

Al Itrah Foundation [3]

Kitabu kilichoko mkononi mwako ni tarjumi kutoka lugha ya Kiarabu ya kitabu maarufu katika ulimwengu wa Kiislamu, Nahju 'l–Balaghah. Kitabu hiki kitachapishwa katika majalada mbali mbali, na hili ulilo nalo mkononi ni jalada la kwanza.

Nahju 'l–Balaghah ni mkusanyiko wa khutba, barua na maelekezo ya Imam Ali (a.s.). Mengi yamesemwa kuhusu ubora na ufasaha wa maneno yaliyomo katika khutba na harua hizo. Kwa ufupi, Nahju 'l–Balaghah ni kilele cha ufasaha.

Translator(s):

Shaikh Harun Pingili [4]

Compiler(s):

Ustadh Abdul–Karim Nkusui [5]
Dr. Ja'far A.Tijani [6]
Ramadhani Kanju Shemahimbo [7]

Category:

Imam Ali [8]

Topic Tags:

Khutba [9]

Barua [10]
Risala [11]

Person Tags:

Imam Ali (as) [12]
Mtume Muhammad (s.a.w) [13]

Neno La Mchapishaji

Kitabu kilichoko mkononi mwako ni tarjumi kutoka lugha ya Kiarabu ya kitabu maarufu katika ulimwengu wa Kiislamu, *Nahju 'l–Balaghah*. Kitabu hiki kitachapishwa katika majalada mbali mbali, na hili ulilo nalo mkononi ni jalada la kwanza.

Nahju 'l–Balaghah ni mkusanyiko wa khutba, barua na maelekezo ya Imam Ali (a.s.). Mengi yamesemwa kuhusu ubora na ufasaha wa maneno yaliyomo katika khutba na harua hizo. Kwa ufupi, *Nahju 'l–Balaghah* ni kilele cha ufasaha.

Mbali na mawaidha yaliyomo humo, msomaji atafaidika na lugha iliyomo katika khutba na barua hizo, hususan kwa wasomaji wa Kiarabu.

Inasemekana kwamba baada ya Qur'ani Tukufu na maneno ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w), *Nahju 'l–Balaghah* ndiyo inayofuatia kwa ufasaha na ubora wa maneno.

Si rahisi kwa msomaji wa Kiswahili kupata ladha ileile aipatayo msomaji wa Kiarabu kutokana na ukweli kwamba lugha ya Kiarabu ni pana mno na msamiati wake ni mkubwa. Pamoja na hayo, mtarjumi wetu amejitahidi sana kuleta maana ya maneno ya Kiarabu kwenye lugha ya Kiswahili bila kupoteza maana yake.

Kwa vile kitabu hiki ni muhimu sana, tumeona ni bora tukichapishe katika lugha ya Kiswahili ili Waislamu na wasomaji wetu wazungumzao Kiswahili wapate kunufaika na yaliyomo humo. Hivyo, ni matumaini yetu kwamba kitabu hiki kitakkuwa ni chenye manufaa sana kwao na katika jamii yetu.

Tunamshukuru ndugu yetu, Sheikh Harun Pingili kwa kukubali jukumu hili kukitarjumi kitabu hiki. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwa kitabu hiki.

Mchapishaji
Al–Itrah Foundation
S. L. P. 19701

Dar-es-Salaam, Tanzania

Dibaji

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema Mwenye Kurehemu. Kwanza yanipasa nimshukuru Mwenyezi Mungu Jalali, asiye kuwa na mithali, kwa neema zake za kila hali na kila mahali, hata nikaweza mimi mja mpungufu, kutimiza kazi hii tukufu ya kuipitia tarjuma hii ya Kiswahili ya Nahju 'l-Balaghah.

Nahju 'l-Balaghah ni jina la diwani mashuhuri yenye khutba, uweza wa kusema, na barua za Imam Alî bin Abu Talib (a.s.). Haya yote yamekusanywa na Sharîf Ar-Radhi. Diwani hii yenye khutba takriban 237, baru 79 na mithali 480 ilikamilika mwezi wa Rajab 400 A.H./1009 A.D. Maana ya NAHJ ni njia iliyo wazi, au barabara kuu; na maana ya Balaghah ni ufasaha (wa lugha) au ilimu ya usemaji, n.k. Kwa hivyo *Nahju 'l-Balaghah* yaani Barabara kuu ya ufasaha.

"Huyu Imam 'Ali ni nani? Ni vigumu mno kuzitaja sifa zake kwa ukamilifu. Yeye alikuwa mtaalamu, shujaa na khatibu kuliko wote. Uchamungu wake, mapenzi yake ya Mwenyezi Mungu, uaminifu wake na ushupavu wake wa kufuata dini ulikuwa wa darja ya juu kuliko mtu yeyote ..... akichukia diplomasia (ujanja), na akipenda haki na insafu. Sera zake ni kama zilivyoamrishwa na Mwenyezi Mungu. Wataalamu wa Kiyahudi na wa Kikristo wakijaaliwa kujua daraja ya ilimu yake huisujudia ilimu hiyo isioweza kufananishwa.

Wafalme wa Ki-Rumi wangependa kuzitundika picha zake katika kasri zao, na maaskari wakubwa wa vita wangependelea kulichonga jina lake kwenye panga zao.

لآ فتي ا لاَّ عَلِيَّ وَ لآ سَيْفَ اِلاَّ دُ و الْفقار

"Hayuko kijana shujaa mfano wa 'Ali! wala hakuna upanga mfano wa Dh-ul-Faqar* (*upanga wa Imam 'Alî* (*a.s.*) *aliorithi kwa Mtume*).*"

Allama Mustafa Beck Najeeb wa al-Azhar, Cairo amesema:

خَرَجَ اِلَي الدُّ نْيَا وَ الثَّهَادَةُ مَكْتُوْبَةٌ عَلي جَبَيْنِهِ وَ خَرجَ مِنْهَا وَ الثَّهَادَةُ مَكْتُوْبَةٌ عَلي
دَ لِكَ الجَبَيْن بضَرْبَهِ حُسًّا م لَقدْ كَمَا عَلِمْنَا فِي الْكَعْبَهِ وَ ضُربَ كَمَ عَلِمْنَا فِي
الْمَسْجِدِ قأَيَّه بَدَايَهٍ وَ نِهَايَهٍ اَثْبَهً بالْحَيَاةِ الّتي بَيْنَهُمَا مِنْ تِلْكَ الْبدَايَهٍ وَ تِلْكَ النَّهَايَهِ؟

"Imam 'Alî amekuja duniani na shahada imeandikwa kwenye kipaji chake; na ameondoka duniani na shahada vile vile imeandikwa kwenye hicho kipaji kwa dharba ya upanga. Kama tunavyojua amezaliwa ndani ya Ka'bah, na kama tujuavyo amepigwa dharba (ya upanga) msikitini. Ilioje ajabu? Mwanzo wake na mwisho wake kupata darja ya kifo cha kishahidi."

Sheikh Abbas Mahmud al–Aqqad – mwandishi maarufu wa Ki–masri amesema:

"Mtu yeyote ambaye amebobea katika lugha ya Ki–arabu atakubali tu kwamba *Nahju 'l–Balaghah* inafuata kwa ubora wake baada ya maneno ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Maneno ya 'Alî ni yenye maana na fikra nzito. Kwa hivyo *Nahju 'l–Balaghah* lazima isomwe kwa makini, na irejewe na idondolewe na wanafunzi na walimu. Ninapenda kutilia mkazo kwamba *Nahju 'l–Balaghah* iingizwe kwenye mukhtasar wa masomo na mafundisho (syllabi) ya vyuo vikuu vyote vya Masri na Beirut kwenye masomo ya kiwango cha juu ya lugha na falsafa."

Sheikh Muhammad 'Abdo – Mufti wa Masri na Profesa wa lugha ya Kiarabu na falsafa amesema:

تَحْتَ كَلاَمِ الْخَالِق وَ فَوْقَ كَكَ مِ الْمَخْلُوق

"Mtu yeyote hawezi kukataa kwamba 'Alî alikuwa Imamu wa makhatibu, mwalimu na kiongozi wa waandishi na wanafalsafa. Bila ya shaka khutba zake na maneno yake ni yenye kiwango cha juu kabisa kushinda maneno ya mtu ye yote isipokuwa maneno ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake:"

'Abd–ul–Masîh al–Antaqi – Mhariri wa Kikristo wa gazeti la Ki–masri Al– Ahram amesema:

'Alî alikuwa Imamu kwenye nyanja za vita, Imamu wa siasa, Imamu wa dini, Imamu wa falsafa, Imamu wa maadili, Imamu wa maandiko mbali mbali, na Imamu wa ilmu na hikma."

Profesa Muhammad Kamil, Cairo amesema:

فاِ دَا لَمْ يَكُنْ عَلِيٌّ نَبِيًّا فلَقدْ كَانَ خُلُقُهَ نَبَو تًّا

"Ijapokuwa Imam 'Alî alikuwa si nabii, lakini khulqa yake ilikuwa ya kinabii."

Shaykh Nasif al–Yazidi alipokuwa akimwaidhi mwanawe alimwambia: “Kama unataka mamlaka ya juu kabisa dhidi ya wenzako katika masomo, hikma, maandiko, inshaa n.k. basi hifadhi Qur'ani Tukufu na *Nahju 'l– Balaghah*”.

Amîn Nakhlah anasema: “Mtu yeyote anayetamani kuikata kiu yake (ya kiroho) kwa maneno ya 'Ali (a.s.)

lazima ausome kila ukurasa wa *Nahju 'l– Balaghah* kwa uangalifu.

Nahju 'l–Balaghah ni diwani ambayo humfanya kila mtu kuukubali ubingwa wa Imam 'Ali (a.s.). Hakuna kitabu kinachoweza kuishinda *Nahju 'l– Balaghah* isipokuwa Qur'ani Tukufu. Humo ndani ya *Nahju 'l–Balaghah* utazikuta lulu za maarifa zilizotungwa kwenye mikufu mizuri, utayakuta maua ya lugha ambayo huifanya akili ya binadamu inukie kwa harufu nzuri ya ushujaa na uungwana; vile vile humo utaikuta mito ya lugha safi ambayo ni mitamu na baridi zaidi kuliko mto wa al–Kauthar.

Imam 'Alî (a.s.) anawaidhi juu ya maudhui mbali mbali, k.m. Kuumbwa kwa ardhi na mbingu, tawhîd, taqwa, malaika, zuhd, Qiyamah, kiburi, tamaa, vita vya Jamal, Siffin, Nahrawan, ibada, maarifa, tamaa, imani, insafu, n. k.

Katika mithali yake mashuhuri Imam 'Alî (a.s.) anatuwaidhi sisi wanaadamu kutobaguwana kwa makabila.

"Watu kwa makamu ni sawa sawa
Baba ni Adamu na mama Hawa
Ukijia'dhimu kwa kuzaliwa
Maji na kinamu uliumbiwa
Fahamu na jua mwana Adamu"

Maneno haya ya Sayyidna 'Alî yamo katika msingi wa Qur'ani Tukufu. (Sh. 'Alî Muhsin al–Barwani).

Tunatumai wasomaji wetu watastafidi sana na tarjama hii ya *Nahju 'l–Balaghah* (kwa lugha ya Kiswahili) ambayo imefanywa kwa kifundi na ujuzi mkubwa. Mwenyezi Mungu atujaalie tawfiq ya Kutenda Kheri na atuepushe na kila shari.

Wa Billahi Tawfîq,
Dr. Ja'far A. Tijani
May 2007

A. Kauli kukhusu nasaba ya amirul–mu'minina ali (a.s) na kutaja sehemu kidogo ya fadhaili zake

Yeye ni Abul'Hasan Ali bin Abi Taalibina jina lake Abdu Manaf bin Abdulmuttalib – na jina lake ni: Shaybatul'hamd bin Hashim–na jina lake ni Amr bin Abdu Manaf bin Qusayyi. Kuniya ambayo aghlabu hutumika kumuita ilikuwa: Abul'hasan.

Na mwanawe Hasan (a.s) katika zama za uhai wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alikuwa akimwita Abulhusayn, na Husayn (a.s) alikuwa akimwita Abulhasan, na wawili hao walikuwa wakimwita Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) baba yao, na alipokufa Nabii (s.a.w.w.) ndipo walimwita baba yao baba.

Na Mtume wa Mwenyezi Mungu alimpa kunia ya: Abu Turab, hivyo ni kwa sababu siku moja alimkuta amelala usingizi kwenye mchanga, hali ikiwa ridaa–nguo–yake imemdondoka, na mchanga ukawa umemtapakaa mwilini mwake. Akamjia na akaketi karibu ya kichwa chake, na alimwamsha na akawa yuampangusa mchanga toka mgongoni huku akimwambia: “Kaa; kwa hakika wewe ni Abu Turab” na tokea hapo ikawa miongoni mwa kunia aipendayo mno katika kunia zake (a.s). Alikuwa ana– furahi kuitwa kunia hii (Abuturab).

Na Bani Umayyah walikuwa wakiwaraghibisha makhatibu wao wamtukane kwa kunia hii wakiwa juu ya mimbari, na waliifanya kuwa ni upungufu fulani na ni dosari kwake; Basi ikawa kwake kama wamemvika pambo, kulingana na alivyosema Hasan Albasri (r. a). Jina lake la kwanza ambalo mama yake alimwita ni: Haidara, ikiwa ni jina la baba yake Asad bin Hashim – na Alhaidara ni: Simba, baba yake (yaani Abutalib) alimbadilisha jina hilo na akamwita Ali. Na kuna kauli isemayo kuwa: Haidara ni jina ambalo Makurayshi walikuwa wana mwita. Kauli ya kwanza ndio sahihi; kwa kuwa kuna habari yajulisha hivyo kutokana na yeye mwenyewe, siku alipomkabili Marhab ambaye alikuwa anajigamba kutafakhari akisema: “Ana lladhi sammatni ummi Marhaba” ndipo hapo Imam Ali (a.s) alimjibu na kumkabili: “Ana lladhi sammatni Haidara”.

Jina la mama yake ni Faatima binti Asad bin Hashim bin Abdi Manaf bin Qusayyi, ni (mwana mama wa kwanza Hashimiya amezaa kwa Bwana wa kihashimii; Ali (a.s) alikuwa mdogo katika watoto wake (huyu mama), na Ja’far alikuwa mkubwa kuliko yeye kwa miaka kumi, na Aqiil alikuwa mkubwa kuliko yeye kwa miaka kumi, na Talib ni mkubwa kuliko Aqiil kwa miaka kumi, na Fatima binti Asad mama wa hao wote.

1. Khutba Ya Kwanza

Ameieleza khutba hii Al’Waasiti ndani ya Kitabu chake (*Uyunul’Mawaaidhi wal’Hikami*), na Az–Zamakh’shari ndani ya (*Rabiiul’Abrari*) mlango wa mbingu na nyota. Na Ibun Shu’uba Al’Halabi ndani ya (*Tuhaful’Uquli*), na Al’Qaadhi Al’Qadhaa–i ndani ya (*Dusturu maalimil’Hikamis*), na Ibnu Tal’ha Ash – Shaafi’i ndani ya (*Matalibus Su’ul*) na Al’Fakh’rur Raazi ndani ya juzu ya pili ya Tafsyri yake.

Ndani ya khutba hii anaelezea kuumbwa kwa ardhi, mbingu, na kuumbwa kwa Adam (a.s)

Anayestahiki sifa njema ni Allah (s.w.t) ambaye ubora wa sifa zake hawa ufikii wasemaji. Ambaye neema zake wahasibu hawawezi kuzihisabu. Wenye juhudi hawawezi kutekeleza haki ya utii wake.

Ambaye fahamu ya hali ya juu ya wenye akili haiwezi kumfikia kumtambua,1 wala, utambuzi wa kina hauwezi kumuelewa 2 ambaye sifa zake hazina mpaka wenye kikomo,3 wala hana sifa.

Wala wakati uhisabiwao, wala muda uliowekwa.4 Ameumba viumbe kwa uwezo wake, na ameutawanya upepo kwa rehema zake; kwa milima ameimarisha uyumbaji wa ardhi yake.

La kwanza katika dini ni kumtambua yeye,5 na ukamilifu wa kumtambua ni kumsadiki, na ukamilifu wa kumsadiki ni kumpwekesha.6

Na ukamilifu wa kumpwekesha ni kumtakasa na ukamilifu wa kumtakasa ni kumuepusha mbali na sifa. Na mwenye kumsifu Mwenyezi Mungu swt. Atakuwa amemuambatanisha,7 na mwenye kumuambatanisha amemfanya kuwa wawili,8 na mwenye kumfanya kuwa wawili atakuwa amemfanya kuwa mwenye sehemu sehemu, na mwenye kumfanya kuwa mwenye sehemu sehemu atakuwa hamjui (s.w.t.), na asiyemjua atakuwa amemuonyesha, na mwenye kumuonyesha atakuwa amemwekea mipaka,9 na mwenye kumuwekea mipaka atakuwa amemuhisabu.10 Na mwenye kusema yuko ndani ya nini? Anakuwa amemwingiza (s.w.t) ndani ya kitu.11

Na mwenye kusema yuko juu ya nini? Atakuwa amemtoa humo.12 Amekuwa yupo sio kwa kutukia, yupo lakini sio kwa maana ya hakuwapo hapo kabla. Yuko pamoja na kila kitu si kwa mwambatano wa kimwili.13 Yutafauti na kila kitu si utafauti wa kimwili, mtendaji sio kwa maana ya harakati za kimwili na vyombo, mwenye kuona pindi hakuna wakuonwa kati ya viumbe wake. Yu pweke pindi hakuna mkazi analiwazika naye wala haoni ukiwa kwa kukosekana kwake.

A. Kuumbwa Kwa Ulimwengu.

Alianza kuumba viumbe mwanzo, na kuvibuni kwa ubunifu, bila ya kupitisha fikra, wala kufaidika na uzoefu wowote, wala hakufanya harakati yeyote, wala kusumbuliwa na azma ya ndani ya nafsi, amevitoa viumbe (kutoka hakuna kitu na kuviingiza) kwenye ulimwengu wa kuwepo kwa wakati wake. Akaviunganisha viumbe pamoja na tofauti zao. Akaweka silika zao, na akaziambatanisha hizo silika na wenyewe. Akiwa mjuzi (s.w.t) kabla hajabuni (viumbe) akiwa mwenye kuelewa kwa ukamilifu, mipaka yao na mwisho wao, akiwa mwenye kutambua utashi wao na sehemu zao nyingi.

Kisha aliumba (s.w.t.) mwanya wa anga na eneo la mbingu na utando wa upepo, alimimina humo maji ambayo mawimbi yake yalikuwa makali na mawimbi yalilundikana moja juu ya jingine, aliyabebesha kwenye upepo uendao kwa kasi, na mtikisiko mkali, na kimbunga kinachovunja. Aliyaamrisha yamwage (mvua) aliufanya upepo uwe na uwezo wa kuzuia nguvu za mvua na kuijulisha mipaka yake. Upepo ulivuma chini hali maji yalibubujika kwa kasi kwa upande wa juu.

Kisha (s.w.t.) aliumba upepo ambao ulifanya mvumo wake uwe tasa. Yaani mvumo wa hewa ulifanywa usioweza kurutubisha kizazi, kwa kuwa kuna upepo urutubishao mimea na kuifanya itoe mazao. Na upepo huu uli- umbwa ili kuyatikisa maji tu. Na akadumisha kubaki kwake, mwendo wake ulishika kasi na akayatawanya kwa umbali na kwa upana.

Kisha aliuamrisha upepo kuyanyanyua maji yalio kwenye kina, na kuongeza kasi ya mawimbi ya bahari.

Yakatikisa mtikiso kama ule ufanywao kwa kinywaji cha maziwa. Na kuvuma nayo angani. (Anakusudia kueleza kuwa upepo ukivuma angani anga ambazo ziko tupu huwa mvumo wake mkali kwa sababu ya kutozuilika na kitu chochote, na upepo huu ulivuma na maji mengi mvumo mkali sana).

Wayarudisha ya mwanzo nyuma na yaliyotulia kuyapeleka kwa yaliyo kwenye mtikisiko, mpaka yakainuka mwinuko. Na sehemu ya chini ilijaa povu. Baadaye Mungu (s.w.t.) aliinua povu lile juu ya upepo ulio wazi kutoka humo aliumba mbingu Saba. Na sehemu ya mawimbi ya chini aliyazuia na kuwa kituo, na ya juu kuwa kama dari inayo zuia na jumba lililoinuka bila ya nguzo zenye kulikinga, wala misumari inayo imarisha, kisha alizipamba (mbingu) kwa mapambo ya nyota na mianga yenye nuru. Na alipitisha humo jua lenye taa yenye kuenea mwanga wake. Na mwezi wenye nuru katika sayari zinazozunguka. Na dari inayokwenda, na ubao uendao.14

B. Kuumba Malaika.

Kisha aliumba mwanya kati ya mbingu za juu na kuzijaza malaika wake wenye daraja tofauti.15

Malaika amewafanya wa aina tatu:

a. Mabingwa wa ibada, miongoni mwao kuna ambao wamesujudu na wala hawarukuu, na kuna waliorukuu na wala hawasimami, kuna waliosimama katika safu na wala hawatawanyiki kuna wanaosabihi na wala hawachoki, hawasinzii, wala hapitiwi, wala hawanyong'onyei, wala kughafilika kwa kusahau.

b. Miongoni mwao kuna waaminifu wa wahyi wa Mungu, na ni ndimi zitamkazo ndani ya vinywa vya mitume Wake, na wanaopokezana kwa hukumu na amri zake (kupitia wao Mungu hupitisha hukumu kwa amtakae kwa apendacho).

c. Malaika wahifadhi wa waja Wake (swt), kana kwamba wao ni nguvu iliyowekwa ndani ya miili ya wanadamu na nafsini mwao. Na miongoni mwao wamo ambao miguu yao imeimarika katika ardhi ya chini, na shingo zao zimechomoza kwenye mbingu ya juu, na nguzo zao zimezidi kwenye peo (horizon), na mabega yamelingana na nguzo za Arshi, wenye kuinamisha macho yao mbali na Arshi, wenye kuizingira kwa mbawa zao, imepigwa pazia ya utukufu kati yao na wasiokuwa wao na stara ya uwezo, hawamfanyii taswira Mola wao, wala hawampitishii sifa za viumbe, wala hawamuwekei mipaka ya mahali, wala hawamuashirii kwa mifano.

C. Maelezo Ya Kuumbwa Kwa Adam (A.S.)

Kisha (s.w.t.) alikusanya aina za udongo: Ngumu, laini, tamu, chachu, udongo ambao aliumwagia maji mpaka ukalowana, na aliukanda kwa unyevunyevu mpaka ukaganda, kutoka humo aliumba sura yenye pande tofauti, na viungo tanzu, sehemu ya pingili aliigandisha na ikashikamana, akaifanya kuwa ngumu mpaka ikawa ngumu, kiasi cha kusikika sauti, kwa wakati uliowekwa kwa muda ujulikanao.

Baadaye alipulizia humo roho, akawa mtu mwenye akili imsukumayo, na fikra aitumikishayo, na viungo vya mwili avitumiavyo, na ala zimsaidiazo kubadilisha hali yake, na maarifa ambayo kwayo anatofautisha kati ya haki na batili, akiwa na uwezo wa kuonja, na kunusa, kupambanua rangi, na jinsi yenye mchanganyiko wa udongo wa rangi tofauti, na vitu vyenye kufanana na kuafikiana, vitu vilivyo kinyume na visivyoafikiana. Aina tofauti za mchanganyiko: kama vile joto, baridi, hali ya chepe, ugumu, chuki, furaha.

Mungu (s.w.t.) aliwataka malaika watekeleze ahadi aliyowekeana nao, na kutimiza agizo lake la kuwataka wamsujudie Adamu, na kunyenyekea ili kumpa heshima, akasema (s.w.t): “Msujudiyeni Adamu, walisujudu isipokuwa iblisi”. Quran 2:34. Yeye alijiona, akazidiwa na uovu, akajitukuza na kufanya kibri kwa sababu ya kuumbwa kutokana na moto. Alikebehi asili ya umbo la Adamu, yaani udongo.

Mungu (s.w.t.) alimpa (Ibilisi) muda ili ghadhabu ithibiti kwake. Na kukamilisha mtihani (kwa mwanadamu) na kutekeleza ahadi, akasema: **“Basi kwa hakika umekwisha kuwa mingoni mwa waliopewa muhula mpaka ya siku ya wakati maalum” (15:38, 38:81)**

Baadaye Mungu (s.w.t.) alimuweka Adamu peponi ambapo aliyafanya maisha yake yakuridhisha, na kubaki kwa amani. Alimtahadharisha na Ibilisi na uadui wake. Adui yake (ambae ni Ibilisi) alimghuri. Akimwonea wivu kubaki kwake milele Peponi akiwa na watendao mema. Akauza yakini kwa shaka yake, na azma kwa unyonge wake, na furaha aliibadilisha kwa woga. Na kuhadaika ikawa ni majuto.

Kisha Mungu s.w.t. alimpa Adamu fursa ya kutubia. Alimfundisha neno la rehema Zake. Na alimuahidi kumrudisha kwenye Pepo yake. Alimteremsha duniani kwenye makazi ya mtihani, nyumba ya majaribu, na kuzaa watoto.

D. Kuteuliwa Kwa Manabii

Mungu (s.w.t.) aliwateua manabii katika kizazi chake – watoto wa Adamu (a.s) – akachukuwa kwao ahadi kwa ajili ya wahyi, na kuchukuwa dhamana kwao kwa ajili ya kuifikisha risala – Ujumbe – lakini wengi katika viumbe Wake walivyobadili ahadi ya Mungu walipotosha agizo lake (s.w.t.) kwao wakapuuza haki yake wakamfanyia washirika pamoja naye. Shetani aliwapotosha mbali na kumtambua Yeye. Na aliwaweka mbali na ibada yake.

Aliwatuma kwao Mitume wake, aliwapeleka manabii wake kwao kwa vipindi: Ili watekeleze ahadi ya kuumba kwao, na wakumbushe neema zake zilizosahauliwa, na ili watoe hoja kwao kwa kufikisha ujumbe. Ili kuamsha vipaji vya hikima vilivyofichikana. Na kuwaonesha alama za uwezo wake wa kila kitu kama vile mbingu zilizoinuliwa na ardhi iliotandikwa chini yao, na sababu za maisha zinazowapa uhai, na ajali zinazowamaliza, na taabu zinazowazeesha na matukio yanayofululiza kwao.

Mungu (s.w.t.) hakuwaacha viumbe wake bila ya nabii mwenye kutumwa, au bila ya Kitabu

kilichoteremshwa, au bila ya hoja ya lazima, au bila ya njia iliyonyooka.
Hawa wajumbe, hawakujihisi kuwa wachache kwa udogo wa idadi yao wala kwa ukubwa wa idadi ya wanaowakadhibisha. Miongoni mwao aliyetangulia humtaja anayefuata baada yake au mfuasi aliyetambulishwa na mtangulizi wake.

Kwa utaratibu huo karne baada ya karne zilipita, vilizaliwa vizazi. Miaka ikapita, mababa walipita na watoto walichukua nafasi.

E. Kutumwa Kwa Muhammad (S.A.W.W.)

Hali iliendelea hivyo mpaka Allah (s.w.t) alipomtuma Muhammad (s.a.w.w.), mjumbe Wake ili kutimiza idadi Yake, na kukamilisha unabii Wake. Akiwa mwenye kuchukua ahadi Yake kutoka kwa manabii, alama zake (s.a.w.w.) zilikuwa mashuhuri, uzao wake ni wa heshima.

Watu wa dunia hii wakati huo walikuwa kwenye itikadi zinazotofautiana, tamaa za nafsi zimeenea, na njia zikiwa tofauti, wakiwemo waliomshabihisha Mungu (s.w.t.) na viumbe Wake au wenye kupotosha jina lake (s.w.t.) au wenye kumshirikisha na viumbe.

Mwenyezi Mungu (s.w.t.) aliwaongoza kupitia kwake kutokana na upotovu, na kwa nafasi yake (s.a.w.w.) aliwaokoa mbali na ujahili.

Kisha Mungu (s.w.t) alimhitari Muhamamd (s.a.w.w.) kukutana naye na alimridhia ili awe karibu Yake (s.w.t), na alimzidishia heshima kwa kumwondoa duniani mahali pa majaribu, kwa hiyo alimchukuwa Kwake kwa heshima (s.a.w.w).

Na aliacha kwenu ambayo manabii waliacha katika Umma zao.16 Kwani hawakuwaacha wamepuuzwa, bila ya kuwaeleza njia iliyowazi, wala watakayoongoka kwayo.

D. Kitabu Cha Mwenyezi Mungu Na Sunnah

Amekuachieni Kitabu cha Mwenyezi Mungu, Mola wenu: kibainishacho halali yake na haramu yake.17 Faradhi zake na fadhila zake. Batilisho (nasikh) zake na zilizobatilishwa (mansukh) zake, ruhusa zake na azma zake, hukumu ambazo ni makhsusi, na ambazo zipo katika sura ya jumla, na ambazo zina mafunzo ndani yake na mithali, ndefu na fupi, thabiti zake na mutashabih zake: zilizo wazi na ambazo ni ngumu kueleweka maana yake, zenye kufasiri aya zilizokuja kwa maana ya jumla, na zenye kubainisha maana zake ngumu. Humo kuna aya ambazo kuzijua ni lazima, na kuna ambazo watu wanaruhusiwa kutozijua.

Na ambazo imethibiti Kitabuni faradhi yake, na zajulikana kutenguliwa katika sunnah, na ambazo ni wajibu katika sunnah kuzitekeleza, na ambazo katika kitabu zaruhusiwa kuziacha.

Na kuna ambazo ni wajibu kwa wakati wake, na wenye kuondoka wakati ujao, uharamu wake pia

watofautiana, kuna ambazo ni kubwa ametishia kwa (kosa hilo) moto wake, au ndogo zenye ghofrani yake, na kati ya yanayokubalika uchache wake na yenye wasaa katika umbali wake.

Kuna ambazo uchache wake wakubaliwa (kwa Mungu) na zenye uwezekano wa kutanuliwa (hukumu yake)18

E. Ndani Ya Khutba Hii Aelezea Hijja

Na amewajibisha juu yenu kuhiji nyumba yake tukufu, ambayo ameifanya ***Qibla*** kwa wanadamu, wanaiendea kama wanyama walazimikapo kuyaendea manyweo ya maji wanayahamanikia uhamanikaji wa njiwa.

Mungu (s.w.t.) ameifanya (Kaaba) iwe ndio alama ya unyenyekevu wao kuunyenyekea utukufu Wake, na utii wao kwa enzi Yake. Amechagua kutoka kwa viumbe Wake watiifu walioitikia wito wake. Na wamesadikisha neno Lake. Na wakasimama msimamo wa manabii Wake. Wakashabihiana na malaika wake wazungukao Arshi Yake. Wanafaidika na biashara ya ibada yake. Wakiharakia kwenye ahadi ya msamaha Wake. Mungu (s.w.t.) ameifanya (nyumba hii) kuwa ni alama ya Uislamu na ni lengo la heshima kwa wanaojikinga nayo.

Amefaradhisha haki yake, na kulazimisha kuihiji. Na amefanya faradhi juu yenu kuiendea aliposema (s.w.t.): **“Na kwa ajili ya Mwenyezi Mungu imewajibikia watu wahiji kwenye Nyumba hiyo, kwa yule awazae njia ya kwendea. Na atakayekanusha basi Mwenyezi Mungu si mhitaji kwa walimwengu. (3:97)**

---

1. Anakusudia hima ya wenye uoni na wanafikra japo iwe ya hali ya juu haiwezi kumdiriki yaani kumtambua (swt) kama kitambuliwavyo kiumbe, wala kumzunguka.
2. ni wingi wa yaani kutambua kuzama mbizi, na hapa maana inakuwa: kuzama mbizi ndani ya bahari ya mambo yazingatiwayo kiakili ili kudondoa lulu za ukweli wa mambo, nazo japo ziende mbali katika mbizi haziwezi kuipata hakika ya dhati yake (swt).
3. Ambaye sifa zake hazina mpaka ujulikanao: yaani sifa hapa yakusudiwa dhati yake na hakika yake (s.w.t.) na jinsi alivyo yaani dhati yake (swt) haina mpaka uwezao kutambuliwa. Amemaliza maneno kuihusu dhati yake (swt) na kuzuilika kwa akili ya mwanadamu kuidiriki, baada ya hapo anazitakasa sifa zake (swt) kuwa hazifanani na sifa za vizushi yaani viumbe vilivyo zuka (hapo kabla havikuwa na baada ya kuumbwa vikawa ndio maana ya kuzuka hapa) kwa hiyo kila sifa za kiumbe kwa kawaida kiumbe huwa na sifa ya (imkaanu) kwa maana ya kuwa kwa kiumbe si wajibu bali ni mumkinul wujudu (kupo ndani ya uwezekano) na Mungu ni wajibul'wujud. Hivyo basi kila sifa za kizushi ina kikomo kama tunavyojiona ndani ya uwezo wetu, ilimu yetu kwa mfano. Kwa kuwa kila moja ina kikomo haiwezi kukivuka, lakini uwezo wa Mungu, ilimu yake haina mpaka kwa uene- vu wake. Hivyo hivyo husemwa kukhusu sifa nyingine za ukamilifu. Na (naat) huwa sifa zinazokubali kubadilika, na sifa zetu zina (naat). Kama vile uhai wetu kwa mfano una daraja kutokea daraja ya mtoto mchanga mtoto wa makamo na daraja baada ya hapo, kama vile wakati wa nguvu, udhaifu, na hali ya wastani, na uwezo wetu pia ni kama hivyo. Na ilimu yetu ina duru ya upungufu na ukamilifu, hali ya undani, na ya uwazi. Lakini sifa zake (swt) zimetakasika mbali na (nautu) kama hizi na -mfano wake, kisha hizi sifa zake (swt) ni azaliza milele hazina hisabu ya wakati wa kuwa kwake na yeye kusifika kwa dhati yake nazo, wala haziwekewi muda.
4. . Wala muda uliowekwa, ni ishara ya kanusho kwa wanaodai kuwa Mungu (s.w.t.) atajuli kana alivyo atakapoonekana

siku ya Kiyama kwa hiyo asema (a.s): Hapana wakati kamwe Mungu atakuwa ajulikana dhati yake.
5. Mwanzo wa dini ni kumtambua Mungu (swt): kwa sababu taq'liid ni batili, la kwanza katika wajibu za kidini ni kutambua. Msingi wa dini ni kumtambua Mungu, na Yeye anaweza kutambuliwa kuwa muumba wa ulimwengu, bila ya kumtakasa, kwa hiyo huo ni utambuzi pungufu, na ukamilifu wake ni kumsadiki dhati Yake kwa sifa makhsusi ambazo yeyote hashirikiani Naye, nayo ni sifa ya wajibu wa kuwepo kwake (wajibul'wu–jud). Na kusadiki huku hakukamiliki mpaka kuwe na lazima yake, nayo ni Tawheed kwa kuwa ambaye kuwepo kwake ni wajibu hana idadi, kama ijulikanavyo katika fani ya Ilahiya na ilmul'kalam (scholasticism). Na Tawheed haikamiliki ila kwa kumtakasia siri kuwa ni yake bila ya kumuambatanisha na kitu chochote miongoni mwa mambo ya matukio katika kumuelekea na kutarajia mwanga wa nuru Yake. Utakaso huu hauwi kamili mpaka uwe pamoja na kumuepushia sifa za dhahiri katika ainisho zionekanazo katika vitu. Kwa sababu kuitambua dhati iliyo takasika ndani ya sifa hizo ni kuizingatia dhati na kitu kingine mbali nayo. Kwa hiyo ametambuliwa (Allah) mwenye viungo na siye Aliye kamili bila ya viungo. Kwa hivyo inakuwa sifa zinazo kanushwa na kutoambatanishwa Naye (swt) ni sifa za viumbe, vinginevyo maneno ya Imamu yamejaa sifa Zake swt. Bali katika maelezo haya amsifu kwa sifa kamilifu mno.
6. Ukamilifu wa kumsadiki ni kumpwekesha: Kwa sababu kujua kuwa Yeye kuwepo kwake ni wajibu peke yake ni kusadiki kupungufu, na kusadiki kamili ni kujua Upweke Wake swt.
7. Na mwenye kumsifu Mwenyezi Mungu atakuwa amemuambatanisha: Kwa sababu mwenye kusifiwa huambatana na sifa, na sifa inamuambata yeye.
8. Na mwenye kumuambatanisha amemfanya wawili kwa hakika, kwa kuwa ame– wathibitisha wa zamani wawilina kufanya hivyo ni kuwafanya wa milele wawili.
9. Kwa kuwa kila chenye kuoneshwa ni chenye mipaka, kwa kuwa wakionyesha kitu kikiwa kipo upande mwingine mbali na ule uliokuwapo, kwa hiyo wewe wakielekea kwa ishara yako. Na ambaye yuko upande fulani anakuwa amejitenga na mwingine, na anakuwa ndani ya mipaka maalumu, yaani kuna ncha anayoishia. Hivyo basi mwenye kumwonesha amemuwekea mipaka.
10. Na mwenye kumwekea mipaka atakuwa amamhesabu: Yaani, amemfanya miongoni mwa vitu vinavyotukia.
11. Kwa sababu mwenye kufanya tasuwira kuwa yupo ndani ya kitu atakuwa amemfanya kuwa ni mwili uliojificha mahali, au kitu miongoni mwa vitu visivyo kuwa mwili, (incorporeal)
12. Na mwenye kusema: Yupo juu ya nini? Atakuwa amemtoa nje yake: Kwa sababu mwenye kufanya taswira kwamba Mungu (swt) yuko juu ya Arshi au yuko juu ya Kursiy amemfanya hayupo katika sehemu zisizokuwa hizo.
13. Yuko pamoja na kila kitu, si kwa mwambatano: Yaani anajuwa vitu sehemu sehemu zake kama avijuavyo katika hali ya ukamilifu wake, kama alivyosema (swt): yaani hawawi katika siri watu watatu ile Yeye ni wanne wao. (Suratul–Mujadillah:7).
14. Sayari zimeitwa ubao kwa kuzifananisha na ubao kwa sababu zipo katika umbo la ubapa.
15. Malaika wabeba Arshi, wao ni kama nguvu ya jumla ambayo Mungu ameikabidhi kwa ulimwengu wote, hiyo ni nguvu inayoushika ulimwengu, na ya uhifadhi sehemu zake zote na makao makuu yake na mipaka ya mwendo wake ni katika mzunguko wake, kwa hiyo nguvu hiyo yapenya na yenye kuingia humo, yenye kuchukuwa kutokea juu yake mpaka chini yake, na kutoka chini yake mpaka juu yake. Na kauli yake: Al'maariqatu minas samaai, al'muruqu: Al'khuruju – kutoka – Na kauli yake: Al'khaarijatu minal'aq'tari arkanuhum: Arkaanu ni viungo vya miili yao, na maneno hayo ni aina ya mfano ulio wazi kwa waelewao.
16. Anakusudia kubainisha kuwa manabii wa Mungu (s.w.t.) hawakuwaacha watu wao bila ya kitakacho waongoza baada ya umauti wao. Kwa hiyo hivyo hivyo ilikuwa kwa Muhammad (s.a.w.w.) yeye aliuachia Umma wake Kitabu cha Mungu (s.w.t.) kikiwa na kila wahitajialo katika dini yao.
17. Halali yake: kama kula vitu vizuri yaani vya halali, na haramu kama kula mali ya watu wengine kwa njia ya batili. Na faradhi zake: Kama zaka dada wa sala. Na fadhila zake: kama vile sunna zake za sadaka ambazo ujira huwa mkubwa kwa kuzitekeleza, wala si vibaya akizembea mwenye kuzembea, na naasikh zake: zilizokuja kutoa hukumu zaondoa waliokuwanayo wapotovu miongoni mwa itikadi, au kuondoa hukumu zilizokuwa hapo kabla, mfano wa kauli yake (swt):
na mansukhah: Iliyokuwa maelezo ya hukumu hizo, mfano wa kauli yake
na aliyoruhusu: mfano wa kauli yake
na ambazo ni lazima: mfano wa kauli yake
na khaaswa mfano wa kauli yake

na aamah: mfano wa kauli yake: Na mafunzo kama aya ambazo zinatoa habari za umma zilizopita miongoni mwa adhabu: “Tumewateremshia adhabu kwa sababu ya kupinga haki na wakafanya dhulma na uadui”. Na mifano: Kama kauli yake: “Mwenyezi Mungu ametoa mfano wa mja mmilikiwa” (16:75). na “Mfano wa ambaye amekoka moto .....” (2: 17). Na vinavyoshabihiana na hayo mengi.

18. Kurejea kwenye mgawanyiko wa hukumu Kitabuni, al–maq'bulu fii adnaahu al'– muwassau fii aqswaahu,: mfano wa kafara ya kiapo Hukubaliwa uchache wake kuwalisha masikini kumi, na ina wasaa katika kuwavika na kumuacha mtumwa huru.

2. Miongoni Mwa Khutba Zake (A.S)

Baada Ya Kutoka Kwake Siffiini

Namuhimidi yeye (s.w.t.) nikiomba utimilifu wa neema Zake, na kusalimu amri kwa utukufu Wake, na kujihifadhi na maasi yake, Namwomba msaada nikiwa mwenye haja ya toshelezo Lake: Kwa hakika hapotei aliyemwongoza, wala hajinasui mwenye kumfanyia uadui.

Wala hawi fukara mwenye kutoshelezwa na yeye. Kwani kumhimidi ni kuzito mno katika mizani na ni hazina bora. Na ninashuhudia kuwa hapana mungu isipokuwa Allah, Peke yake hana mshirika, ushuhuda uliotihaniwa wenye ikhilasi hali ya kuitakidi uhalisi wake.

Tunashikamana nayo shahada milele kwa kadiri atakavyotubakisha, na tunaihifadhi kwa ajili ya hofu itakayotupata, kwa sababu ni azma thabiti ya imani, na ni ufunguo wa mema na radhi ya Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, na ni sababu ya kuwa mbali na Shetani.

Na ninashuhudia kuwa Muhammad ni mja Wake na mjumbe Wake, amemtuma na dini mashuhuri, na sheria iliyonukuliwa, na Kitabu kilichoandikwa, na nuru yenye mwanga, mwanga wenye kuangaza, na amri iliyo wazi, ili kuondoa shaka, na kutoa hoja kwa ubainifu, na kutahadharisha kwa alama, na kuhofisha kwa adhabu.

Na watu wapo katika fitna ya moja kwa moja. Kuna kamba ya dini, na nguzo ya yakini imetetereka, Misingi imetofautiana, mambo yalikuwa yamevurugika, njia ya kujinasua ilibana. Upenyo uliingia giza, mwongozo ulikuwa haujulikani, upofu ulienea.

Mungu mwingi wa rehema walimuasi, Shetani akanusuriwa, imani ilitelekezwa, kwa hiyo nguzo zake zikaporomoka. Mafunzo yake yakabadilika na njia mitaa yake iliharibika.

Walimtii Shetani wakafuata mwenendo wake, wakapita mapito yake, kwao wao alama zake zilipita, bendera yake ikasimama katika fitina, iliyowakanyanga kwa kwato zake, hivyo wao wamepotea wanatangatanga, wajinga wamefitiniwa, wakiwa ndani ya nyumba bora na majirani waovu.1Usingizi wao

ni kukesha, na wanja wao ni machozi.2

Hali ya kuwa wako katika ardhi ambayo mwanachuo wake huzibwa kinywa,3 na jahili wake huheshimiwa.4

Ndani ya khutba hii pia aliashiria kwa aali zake Nabii alayhi Salaatu Wassalaamu: Wao ni mahali pa kuweka siri yake, kimbilio la mambo yake, chombo cha ilimu yake. Marejeo ya hekima zake, pango la vitabu vyake, (*mahali pa kuhifadhia vitabu*) na milima ya dini yake, kupitia kwao Mungu amenyoosha mgongo,5 mgongo wa dini yake, na aliondoa mtetemeko wa viungo vyake.6

Na akawakusudia watu wengine (*wanafiki*): Waliupanda uovu na wakaunyweshea kwa hila na walivuna maangamizi,7 Aali Muhammad (a.s) Hawalinganishwi na yeyote kutika Ummah huu, wala hawawi sawa kabisa nao ambao neema zao zimepitia kwao. Wao ndio msingi wa dini, na nguzo ya yakini. Kwao hurejeshwa mwenye kuvuka mpaka, na kwao huunganishwa aliyeachwa nyuma.8

Haki ya uongozi ni mahususi kwao. Na kwao kuna wasia na urithi; hivi sasa wakati haki imerejea kwa wenyewe, na inahamishiwa mahala penyewe!

---

1. Nyumba iliyo bora ni: Makkah. Na jirani waovu: ni waabudia masanamu miongoni mwa makuraishi.
2. Usemi wake: “usingizi wao ni kukesha, na wanja wao ni machozi” ni kama vile mtu aseme: “ukarimu wao ni ubakhili, na amani yao ni khofu”, yaani lau Muhammad angewaruhusu walale wangebakia bila usingizi badala ya kulala, na lau angewafanya wapake wanja, wanja wao unge kuwa machozi, au wao watakuwa katika matukio ambayo yatawabadilishia usingizi kwa kukesha na wanja kwa machozi.
3. Kauli yake: “kwenye ardhi mwanachuo wake hufungwa kinywa”, yaani, mwenye kutambua ukweli wa Muhammad (s.a.w.w.) na kumwamini, anakuwa katika hali ya taqiyah na woga; kwa kuwa yeye lau atasema ukweli hali jamhuri iko katika batili wangemuuma meno.
4. “Jahili wake huheshimiwa”, yaani, mwenye kuupinga unabii wake na akamkadhibisha, anaenziwa na kulindwa; kwa sababu yeye yupo kama walivyo jamhuri, anakwenda pamoja nao katika utashi wao wa nafsi, daraja yake kwao ni daraja ya dhana zao na ada zao, nazo zikatika daraja la juu nafsini mwao. Na sifa hizi zote ni kuipa taswira hali ya watu katika jahili ya kabla ya kutumwa nabii (s.a.w.w.).
5. Kupinda mgongo ni kinaya cha udhaifu na kuondoa kupindika ni kinaya cha kurejea nguvu ya dini.
6. Ameondoa tetemeko la kiungo chake, farisa ni nyama kati ya upande wa ubavu na bega la mnyama, na kupinda kwa mgongo ni kinaya ya kudhoofu, na kunyoosha ni kinaya ya nguvu, na kwa wao yapatikana amani mbali na khofu, ambayo hutetemesha farisa.
7. Amejaalia waliyoyatenda miongoni mwa maovu ni mfano wa mmea walioupanda, na kutulia kwa nafsi zao kwa kutokuwa na hima na kughurika kwao na hali hiyo ni sawa na kunyeshwea: kwa sababu kughurika kunapelekea kudumu kwa uovu na kuzidi, kisha matokeo ya jambo lao ni haya maangamizi.
8. Anakusudia kuwa sera yao ni Siratud–Din al–Mustaqim, hivyo basi mwenye kuvuka mipaka katika dini yake, wokovu wake ni kurejea kwenye sera ya kizazi chake Mtume, na wajifunike kwa kivuli cha wataalamu wake. Na usemi wake (na kwa wao huunganishwa aliyeachwa nyuma) anakusudia kwamba mwenye kuzembea katika matendo yake, goigoi katika sera yake – ambaye ametanguliwa na waliotangulia – anatamani kujinasua kwa kuinuka ili aungane na kizazi cha nabii na afuate mwendo wao, yaani, yeye Ali (a.s.) amewafanya wao kama kundi la farasi linalotembea kwenye jangwa ambalo wengine ambao wako mbali nalo wapaswa kuungana nalo.

3. Katika Jumla Ya Khutba Zake Alayhis-Salaam:

Nayo ni ile maarufu kuwa ni khutba ya ***Shaq'shaqiyah***.1 "Amma! Wallahi fulani, ameuvaa (Ukhalifa)2 hali akiwa yuajuwa kuwa nafasi yangu kuhu- siana nao ni sawa na mahala pa muhimili wa jiwe la kusagia, maji ya mafuriko huniporomokea wala ndege hawezi kunirukia.

Nilijikinga nao kwa nguo na nikajiweka kando nao. Nikajifikiria, je! Nishambulie na mkono butu, au nilivumilie giza la upofu,3 mtu mkubwa humo huzeeka, na mdogo humo huwa kijana, muumini anataabika humo mpaka akutane na Mola wake, nikaona kuivumilia hali hii ni busara, basi nikasubiri hali jichoni mwangu muna utongotongo, na kooni kuna kitu kilichokwama.

Naiona mirathi yangu imepokonywa,4 wa kwanza akapita katika njia yake, - yaani alikufa - akampasia (ukhalifa) fulani baada yake. **Alinakili ubeti wa kauli ya Al-A'asha -** maana yake: kuna tofauti kubwa kati ya siku yangu nikiwa juu ya ngamia na siku ya Hayyani nduguye Jabir: (yaanni siku ya Hayyani ilikuwa ya raha).

Ajabu ilioje! Alikuwa anaomba wamuuzulu wakati wa uhai wake, punde si punde akaagiza uende kwa mwingine baada ya kifo chake!

Kwa hakika wameshirikiana viwele vyake viwili wao kwa wao tu, huyu mmoja ameuweka (ukhalifa) katika upande ulio mgumu, mguso wake wakwaruza, kujikwaa kunakithiri na kuomba udhuru, aliyekuwa nao ni kama aliyepanda ngamia machachari asiyepandika: akimvuta hatamu atamkaba na akimlegezea atamtupa kweye maangamizi, hapo wallahi watu watapatwa na myumbo, uovu na kupotoka, Nilivumilia kwa muda mrefu wote huo, ingawaje ulikuwa mtihani mgumu: Na alipofikia muda wake akauweka chini ya uchaguzi wa kundi la watu sita akadai akinidhania mimi ni mmoja kati yao. Eee Mungu! Nahusika nini mimi na Shuura!5

Lini ameingiwa na shaka na mimi wa kwanza katika wao kiasi niwe naambatanishwa na mfano wa hawa! Lakini nilitua walipotua, na niliruka waliporuka, mtu miongoni mwao alinigeuka kwa sababu ya kunichukia kwake,6 na mwingine alielemea upande wa shemeji yake.7

Pakiwa na hili na lile, mpaka akasimama watatu wao hali ameinua kifua chake mbele kati ya kinyesi chake na chakula chake - chakula cha mifugo - walisimama pamoja naye watoto wa babu yake, wakawa wanazitafuna mali za Mungu kama anavyotafuna ngamia majani ya msimu wa kuchipua (spring season), mpaka kamba yake ikakatika, na matendo yake yakammaliza, na ulafi wake ukamtupa chini kifudifudi.

Nilishitushwa na kundi la watu likimiminika kuja kwangu mfano wa manyoya ya shingoni mwa fisi toka

kila upande, kiasi kwamba Hasan na Husayn walikanyagwa, na sehemu za ncha za mabega ya vazi langu zikararuriwa, wakiwa wamejikusanya kunizunguka kama kundi la kondoo na mbuzi.

Nilipochukua hatamu za uongozi, kundi moja lilivunja ahadi na jingine liliasi, na lililobaki lilifanya uovu na dhulma8 kana kwamba hawakusikia neno la Mungu aliposema: **"Hayo ndiyo makazi ya akhera, tumewafanyia wale wasiotaka kujitukuza duniani wala ufisadi, na mwisho mwema ni wa wachamungu." (28:83)**.

Ndio wallahi waliyasikia na waliyaelewa lakini machoni mwao dunia ilijipamba na kuliwapendeza kujiremba kwake. Angalia! naapa kwa yule ambaye ameatua mbegu na kumuumba binadamu, lau si kufika kwa watu na kulazimu hoja kwa kuwepo wasaidizi – *yaani askari wa kumnusuru* – na ahadi iliyochukuliwa na Mungu kwa wanachuoni, kuwa wasiridhike kimya kimya na ulafi wa madhalimu na kusagwa kwa haki ya mdhulumiwa, ningeitupa kamba ya ukhalifa kwenye bega lake – *yaani ninge tupilia mbali suala la ukhalifa bila kujali* – na ningemtendea wa mwisho kama wa kwanza. Na mungeona kwa maoni yangu huu ulimwengu wenu si bora kuliko chafya ya mbuzi".

Walisema kuwa: Amirul–Mu'minina alipofikia hapa katika **KHUTBA** hii, mtu mmoja katika watu wa Iraqi alisimama na kumkabidhi karatasi yenye maandishi, akawa anaiangalia, alipomaliza kuisoma, ibn Abbas alimwambia: Ewe Amirul–Mu'minina ungeendelea na **KHUTBA** yako ulipoachia!

Hivyo basi alijibu: "Ewe ibn Abbas hilo ni povu la ngamia, ameunguruma kisha akanyamaza".

Ibn Abbas akasema: "Wallahi sikuwahi kuhuzunikia maneno kamwe, kama huzuni yangu juu ya maneno haya kwamba awe Amirul–Mu'minin hakufikia alipotaka".

Amesema Sharifu (r.a), kauli yake (a.s): *"Ni kama mfano wa aliyepanda ngamia mkorofi":* Anakusudia kuwa, ikiwa atakaza kuvuta hatamu hali akimkinza kichwa chake atararua pua yake, na endapo atamlegezea kitu kidogo na ugumu wake atamuendesha mbio ovyo, na wala hatomdhibiti, husemwa: *Ashnaka naakata* akikivuta kichwa chake kwa hatamu na kukiinua, *na Washanakahaa aidhwan,* pia hutumika kwa maana hiyo*,* hilo limesemwa na ibn Sakiit katika kitabu *Islahu al–Mantiq*. Na sababu ya kusema (a.s) (*Ashanaka laha*) na wala hakusema *Ashnaakaha* kwa kuwa amelijaalia liwe mkabala wa kauli yake: (*Aslasalaha*) hivyo inakuwa kama kwamba amesema: *In raf 'a laha ra'saha bizimami:* yaani ameishika.
Na katika hadithi imekuja kuwa Mtume wa Mungu (s.a.w.w) alihutubia akiwa juu ya ngamia aliyemvuta hatamu kwa kuinua kichwa chake*.* Na miongo– ni mwa ushahidi kuwa (*ashnaka*) maana yake (*Shaanaka*) ni kauli ya Adiyyu bin Zayd al–Abadiyy: *Sa'a aha maa tabaiyyana fil aidi wa ish– nakuhaa ilal–a'anaaqi.*

---

1. Kwa ajili ya kauli yake: (hiyo ni Shaqshaqa hadarat thumma karrat) kama inavyokuja.
2. Fulani ni kinaya ya khalifa wa Kwanza Abu Bakr, (na katika nakala ya Ibn Abi–Hadid: Hakika mwana wa Abi Quhafa ameuvaa). Na ameuvaa: yaani ameufanya kama kanzu naye ameingia humo.

3. Yaani nilivumilia katika giza kwa uchungu kama avumiliavyo mgonjwa wa macho.
4. . Naiona mirathi yangu imepokonywa, ametumia kinaya ukhalifa kuwa ni mirathi, nayo ni mali inayo milikiwa.
5. Msingi wa Shuraa ni kutaka ushauri. Na kisa hiki kwa sura ya jumla ni kwamba: Umar bin Al'Khatab ulipotimia muda wake wa kuiaga dunia, aliwataka ushauri waliokuwa karibu naye kuhusu ni nani amtawaze ukhalifa baada yake! Alishauriwa amtawaze mwanawe Abdullah, akasema:
Hawatotawalia – yaani ukhalifa – wawili katika wana wa al'Khatab, yamtosha Umari aliy– oyabeba. Halafu aliona kuwa aliwakilishe jambo hili kwa watu sita, alisema: (hakika Mtume s.a.w.w. alikufa akiwa radhi nao, na juu yao baada ya mashauriano wamuainishe mmoja miongoni mwao asimamie jambo la Waislam), na watu sita wa Shuura nao ni: Ali bin Abi Talib, Uthman bin Affan, Talha bin Ubaidullah, Zubeir bin Awwam, Abdur–Rahman bin Auf na Sa'd bin Abi Waqqas.
Saadu alikuwa mtoto wa Ami yake Abdur Rah'man wote wawili kutoka bani Zuh'ra, na naf– sini mwake kulikuwa na jambo dhidi ya Ali Karramal llahu Waj'hahu kwa upande wa wajomba zake, kwani mama yake ni Hamnatu binti Sufyani bin Umayyah bin Abdi'Shaamsi. Na Ali ni maarufu mashuhuri kwa kuwa uwa mashujaa wao wa kishiriki– na.Na Abdur Rah'man alikuwa shemejiye Oth'man, kwa kuwa mkewe alikuwa Ummu Kulthum bint Uq'bah bin Abi Muiyt alikuwa dada wa Oth'man bin Affan upande wa mama yake.
Na Tal'ha alikuwa aelemea sana upande wa Oth'man kwa sababu ya mawasiliano yao mema, kulingana na yaliotajwa na baadhi ya wasimulizi wa mambo ya kale. Kwa hiyo kuelemea kwake kwa Oth'man kunatosha kumtupilia mbali Ali, kwani yeye pia ni katika Bani Taymi. Na kati ya Bani Hashim na Bani Taymi kulikuwa na ghadhabu kwa sababu ya ukhalifa wa Abubakar.
Na baada ya kifo cha Omar bin Khattab walikusanyika na kushauriana. Walitofautiana, Talha katika rai yake aliungana na Oth'man, na Zubair akawa upande wa Ali na Saad upande wa Abdur Rah'man.
Inaendelea uk. 19
Na Omar bin Khattab ali usia kuwa muda wa Shuraa usiwe mrefu zaidi ya siku tatu, na kwamba isifike siku ya nne illa tayari wawe na amiri, na alisema Omar: "Ikitokea tofauti munapaswa muwe upande ule wa kundi la Abdur Rah'man." Abdur rah'man Alimkabili Ali na kumwambia : "Ni juu yako ahadi ya Mungu na makubaliano yake utafanya kulingana na Kitabu cha Mungu na Sunnah ya Mtume na makhalifa wawili waliokuwa baada yake" Ali alisema: "Nataraji nifanye kulingana Kitabu, sunna na upeo wa ilimu yangu na uwezo wangu. Kisha alimwita Uthman na akamwambia mfano wa aliyomwambia Ali. (Yeye) Alimwitikia kwa: Naam, kisha Abdur'rah'man aliinua kichwa chake kuielekea dari ya msik– iti – mahali ambapo Shuraa ilikuwa inafanyika – na akasema: (Ewe Mungu Wangu sikia na shuhudia, hakika mimi nimejaalia lililokuwa shingoni mwangu katika shingo ya Uthman) alipiga mkono wake kwenye mkono wa Uthman na akasema: (As–salaam alayka yaa Amiral–Mu'minin) na akamfanyia bai'a.
Wakasema: (Akatoka Imam Ali bin Abi Talib hali amekasirika) Mikdadi bin Al'Aswad akamwambia Abdur'rah'man: (Wallahi umemwacha Ali naye ni miongoni mwa ambao wanahukumu kwa haki na wanafanya uadilifu katika hukumu) akasema: (Ewe Mikdadi kwa kweli nimefuatilia kwa juhudi zangu kwa ajili ya waislamu) Mikdadi akasema: (Wallahi kwa kweli mimi nawashangaa maquraishi kuwa wao wamemuacha mtu ambaye, sisemi wala simjui kuwa kuna mtu anahukumu kwa haki wala mjuzi zaidi kuliko yeye) Abdur'rah'man akasema: (Ewe Mikdadi, mimi nahofia fitna, kwa hiyo mche Mungu).

Kisha yalipotokea katika utawala wa Uthman, yaliyotokea kupatikana kwa matukio toka kwa watu wa karibu yake, wakiwa magavanaa wa mikoa, masahaba wakubwa wakubwa walimchukia. Imeelezwa kuwa yeye alimwambia Abdur'rah'man: (Haya ni matendo ya mkono wako) Akasema: (sikuwa namdhania huyu kuyafanya haya, Lakini namuapa Mungu sitosema naye abadan). Kisha Abdur'rah'mani alifariki akiwa haongei na Uthman, mpaka yasemekana: (kuwa Uthman aliingia kwa Abdur'rah'man wakati yu mgonjwa akimzuru, akageukia ukutani bila kusema naye) Mungu ndiye ajuaye, na hukumu ni ya Mungu, anafanya atakayo. Mwisho wa Tanbihi 31

6. Mtu miongoni mwao hapa anamkusudia Talha.
7. Mwingine alielemea kwa shemeji yake anamkusudia Abdur–Rahman ambaye alielemea kwa Uthmani; kwa sababu Ummu Kulthum bint Ukbah bin Abii Mu'iti alikuwa mke wake Abdur–Rahman. Na huyu Ummu–Kulthumu ni dada wa Uthmani upande wa mama yake Urwa binti Kuraizi.
8. An–Nakithu: Watu wa ngamia, na al–Mariqatu: Watu wa Nahrawan, na al–Qasituna: Wadhalimu, watu wa Siffin, na Maraqat: Kharajat, na katika maana ya kidini: Fasaqat.

4. Na Miongoni Mwa Khutba Zake (A.S)

Hotuba hii ameitoa baada ya kuuliwa Talha na Zubair ili kuwaongoza watu na (*kuwabainishia*) *ukamilifu wa yakini ya ustahiki wa uongozi wake:-*

“Kupitia sisi mumeongoka kutoka gizani[1] na mumepanda daraja ya juu. Na kupitia sisi mumepambazukiwa na alfajiri mkiwa mbali na giza la usiku.

Asiyenisikia, basi lizibe sikio lisilosikia mawaidha. Vipi ataisikia sauti dhaifu na aizingatie aliyefanywa kiziwi (hakuweza kusikia) na ukelele wa sauti kubwa? (Atasikia sauti yangu dhaifu?). Uimarike moyo ulioendelea kumwogopa Allah.

Siku zote nilikuwa natazamia kutoka kwenu usaliti, na nimekuoneni ndani ya pambo la walioghurika, pazia ya dini imewaficheni mbali na mimi. Lakini nia yangu ya kweli imenionesha mlivyo. Nilizisimamisha kwa ajili yenu njia za haki kati ya njia za upotovu, hali ikiwa mlikuwa mnakutana lakini hapakuwa na kiongozi, na mlichimba bila ya kupatikana maji.

Leo navifanya hivi vitu bubu[2]vyenye ubainifu viwasemesheni.

Hana rai mwenye kuwa kinyume na mimi. Sikuwa na shaka na haki toka nilipoonyeshwa! Musa (a.s) hakujihofia binafsi,[3] bali alihofia ushindi wa majahili na zamu ya upotovu! Leo tumesimama njia panda kati ya haki na batili.[4]

Mwenye kuwa na hakika ya kupata maji hawezi kuhisi kiu.[5]

Maelezo: Maneno haya na mifano yamedondolewa kutoka **KHUTBA** ndefu iliyonasibishwa kwake (a.s), kaumu ya watu fulani imezidisha humo vitu, kilichowafanya wafanye hivyo ni utashi wa nafsi zao.

Matamshi hayo hayaafikiani na utaratibu wake (a.s) katika **KHUTBA**, wala ufasaha wa hayo hauendani na ufasaha wake. Wala hapana haja ya kutaja kwa kuwa ni mashuhuri.

Na sisi tutafafanua matamko haya, kwa kuwa ni maneno yake (a.s), hawi na shaka na hilo mwenye *dhouqu* na *naqdu* na kuwa na maarifa na mwenendo wa watoa khutba na wenye ufasaha katika khutba zao na risala zao. Na kwa sababu Ar-Radhiyy (r.a) ameidondoa na ameinasibisha kwake (a.s) na ameisahihisha na kuondoa yasiyo yake.

---

1. Ama kukhusu usemi wake(a.s): (kupitia sisi mumeongoka katika giza): Akusudia giza la ujinga na kupanda kilele: mumepanda daraja. Na ibara hizi ni Istiara-methali.

2. Vitu bubu alikusudia alama na ishara, kwani hizo japokuwa ni bubu kwa asiyeelewa, lakini ziko wazi kwa mwenye moyo wa uelewa (li man kaana lahu kalbu au alqas-sam’a wa huwa shahid) kwa ajili hiyo ameviita vyenye ubainifu ingawaje ni bubu na bubu ni mnyama

3. Anafuata nyayo za Musa pale walipomzulia woga, na anabainisha ukweli wa mambo mbali na wanayoyadhania, hakujihofia nafsi yake, bali alihofia fitna kuingia kwa watu wenye akili timamu pindi walipotupa wachawi fimbo zao, hivyo hivyo mimi sijihofii maadui binafsi ambapo wamenitegea mitego, bali nahofia wasije wakadanganyika wenye akali timamu kwa utata wao, hivyo dola ya upotovu itakuwa na nguvu, neno la wajinga lisije likashinda.
4. Yaani, leo haki na batili zimekuwa wazi na tumezijua sisi na ninyi.
5. Anasema: Mkiniamini mtakuwa mbali na upotovu, na karibu na yakini, kama ambaye ana uhakika na maji katika chombo chake anavyokuwa mbali na kiu, kuliko asiyekuwa na uhakika.

5. Miongoni Mwa Khutba Zake (A.S)

Alipofishwa Mtume wa Mungu (S.A.W.W.):

Abbas na Abu Sufyan bin Harb walimsemesha Ali (a.s) kuwa wamfanyie bai'a ya ukhalifa, ndipo aliposema (a.s): "Oh! ninyi watu; yapasueni mawimbi ya fitna kwa merikebu za uokovu, na jiepusheni na njia za chuki, vueni taji za fahari, atakuwa amefanikiwa mwenye kuinuka na bawa,1 au asalimu amri akapumzisha (akapumzisha nafsi yake au wengine wakabaki salama).

Ni maji machafu,2 na ni tonge limkwamalo mlaji wake, na ni sawa na mchuma matunda kabla ya wakati wa kupevuka kwake,3 na ni sawa na mkulima wa ardhi isiyo yake.

Nikisema mimi watasema: Amepupia ufalme, na nikinyamaza watasema: Amekuwa si mvumilivu wa umauti! haiwi baada ya kale (kafupi) na huyu (mrefu)!4 Wallahi mwana wa Abi Talib ni mchangamfu mno wa mauti kuliko mtoto mchanga anavyochangamkia ziwa la mama yake, isipokuwa nimezingirwa ndani ya ilimu iliyositiriwa, lau ningeifichua mngetetemeka mtetemo wa kamba ya kisima cha ndoo katika kisima kirefu.

---

1. Atakuwa amefanikiwa mwenye kuinuka na bawa: yaani atakuwa ame fanikiwa mwenye kuutafuta uongozi akiwa na msaidizi wa kumsaidia na wanusuru wapiganao mbele yake.
2. Maji machafu: anaishiria kwenye ukhalifa, yaani kwa kweli kuwaongoza watu na kutawalia mambo yao ni miongoni mwa mambo hayamuwii vyema mwenye kuyatawalia, bali hilo ni jambo linashabihiana na kuyatumia maji machafu, matokeo yake hayamfaidishi, ni kama tonge linalomkwama mlaji wake na kufa nalo.
3. Mchuma matunda kabla ya kupevuka: Anaishiria kuwa wakati ulikuwa si muwafaka kulitaka suala lile la (ukhalifa) kwa hiyo lau angesimama kwa ajili hilo angekuwa kama mchuma tunda kabla halijapevuka kwa hiyo hafaidiki na alichochuma, kama ambavyo aliyelima kwenye ardhi isiyo yake hanufaiki na kazi aliyoifanya.
4. "Baada ya kale na huyu" Baada ya kuwa nimeyakabili mambo yakutisha makubwa na madogo, na nimepatwa na kila aina ya masaibu makubwa na madogo, kwa hiyo Kale ni ishara ya msiba mdogo na Huyu ishara ya msiba mkubwa. Na chimbuko la methali hii katika kiarabu, yasemekana mtu mmoja alioa mwanamke mfupi mwenye tabia mbaya kwa hiyo maisha yake na yule mwanamke yalikuwa katika shida na mashaka, baadaye alimtaliki na akaoa mwingine mrefu, taabu na mashaka yake ikawa zaidi, akamta- liki na akasema: "sitoowa baada ya kale kafupi na huyu mrefu" tokea hapo ikawa methali katika shida na masumbuko, makubwa na madogo. Na kauli yake (Hay haata): ni kanusho ambalo wangedhania

kuwa kunyamaza kwake yu ahofia mauti.

6. Miongoni Mwa Khutba Zake (A.S)

Aliposhauriwa kuwa asimfuatilie Talha na Zubair wala – asijiandae kwa vita na wao, pia humo anabainisha sifa yake kuwa yeye (a.s) – hawezi kuhadaiwa, ndipo aliposema:

“Wallahi siwi kama fisi anayelala muda wote wa mdundo mpaka amfike anayemtafuta, na amhadae muwindaji wake.

Lakini mimi nitampiga aigeuziaye mgongo haki kwa msaada wa anayeikubali, na kwa msaada wa msikivu mtii nitampiga, nitampiga muasi mwenye shaka daima, mpaka nijiwe na siku yangu (ya mauti); Wallahi ningali nasukumwa mbali na haki yangu, imetwaliwa kinyume nami toka siku Mwenyezi Mungu (swt) alipomfisha Nabii wake (s.a.w.w.) mpaka siku hii ya leo.1

---

1. Anasema; kwa kweli kutwaa ukhalifa na kujitenga nao dhidi yangu na kuuhodhi si jambo jipya lililotokea hivi sasa, bali lilianzia mara tu alipofishwa Mtume wa Mungu (s.a.w.w.).

7. Miongoni Mwa Khutba Zake (Amani Imfikie)

Katika kuwalaumu wafuasi wa Shetani:

“Wamemfanya shetani kuwa ndio kiini cha mambo yao, na yeye amewafanya washirika wake.

Hivyo basi ametaga na kutotoa vifuani mwao,1 na ametambaa na kujiburuza mapajani mwao,2kwa hiyo aliangalia kwa macho yao, na alitamka kwa ndimi zao, hivyo basi aliwapotosha, na kuwapambia kauli ovu, na makosa mabaya ni kitendo cha ambaye shetani ameshirikiana naye katika mamlaka yake na akatamka ya batili ulimini mwake.”

---

1. Ametaga na kutotoa: ni kinaya (metaphoric), inamaanisha kuchukua nafasi kwake vifuani mwao na kubaki kwake muda mrefu humo; kwa kuwa ndege hatagi isipokuwa ndani ya kiota chake. Na kutotoa kwa shetani ni ule utiaji wake wasiwasi.
2. Kuburuzika mapajani mwao: yaani wao wameilea batili kama wazazi wawili wamleavyo mtoto mapajani, hiyo ni kuonyesha kiwango cha kuambatana kwake nao na kuchanganyika kwake pamoja nao na kuwa kama ambaye anaangalia

kwa macho yao, na yuatamka kwa ndimi zao, yaani wawili wamekuwa kama mtu mmoja.

8. Na Miongoni Mwa Maneno Yake (A.S)

Kwayo anamkusudia Zubair katika hali ambayo ilibidi iwe hivyo:

“Anadhani kuwa amekula kiapo cha utii kwa mkono wake, wala hakula kiapo kwa moyo wake, kwa hiyo amekiri kula kiapo cha utii, na anadai yaliyojificha ndani ya dhamira yake, basi na alete hoja ya kuthibitisha hilo, kama sivyo yampasa aingie alikotoka.”1

---

1. Katika usemi wa Imam: waidda’aa al’waliijah: Al’waliijah: ni jambo lililositiriwa lililofanywa kwa kufichwa. Na Bw. Zubair alikuwa akisema: “Nimefanya bai’a – kiapo cha utii”. Nimekula kiapo cha utii kwa mkono wangu si kwa moyo wangu, au pengine anadai kuwa alilishwa kiapo bila ya ridhaa yake, na pengine anadai kuwa alikula kiapo kwa kujionesha tu kuwa yu ala kiapo, lakini alikuwa hali kiapo halisi. Kwa mantiki hiyo akasema (a.s): Usemi huu ni kukiri Zubair kuwa alikula kiapo cha utii, na yu adai jambo jingine ambalo halina ushahidi, hivyo basi alete dalili ya kuthibitisha kubatilika kwa kiapo alichokula dhahiri, au arejee kwenye utii wake.

9. Miongoni Mwa Maneno Yake (A.S)

Miongoni mwa maneno yake (a.s) – Sheikh Al–Mufiid ameieleza hii ndani ya Kitabu chake (*Al–Jamalu*) kutoka kwa Al– Waaqidiy.

Maelezo yanayomhusu (a.s.) na maelezo ya mahasimu wake, na pengine husemwa kuwa: yanawahusu watu wa Vita vya Jamal (Ngamia): “Kwa kweli waliunguruma na kumulika,1 pamoja na mambo mawili haya ni woga. Sisi hatuungurumi mpaka tushambulie adui na hatutiririki mpaka tunyeshe.2

---

1. Maneno yake sana yalikuwa ya methali. Kwa hiyo kuunguruma na kumulika hapa ni methali ya mtu anayetaka kumshambulia adui, huanza na kelele za vitisho, kabla hajasham– bulia ili kuingiza hofu moyoni.
2. Sisi hatuungurumi mpaka tufanye: yaani hatumtishii adui ila baada ya kipigo, kwa sababu sisi tukishampiga adui tunamtishia mwingine kuwa atasibiwa na lililomsibu wa kwanza. Tukinyesha twatiririka, ama hao ambao wanasema: (tutafanya, tutafanya) wala sio wafanyaji, wao wako sawa na anayetiririka kabla ya mvua, na hivyo ni muhali haupo.

10. Miongoni Mwa Maneno Yake (A.S)

Miongoni mwa maneno yake (a.s)– Al wahihiy ameieleza hii ndani ya Kitabu chake (Al jamaalu).

Katika khutba hii huenda anamkusudia shetani wa kweli, na inawezekana awe anamkusudia Mu'awiya. Ikiwa anamkusudia Mu'awiya basi kauli yake: (qadjama'a …) ni maneno yapitayo juu ya ukweli wake, na ikiwa anamkusudia Shetani huo utakuwa ni mlango wa istiara.

Au kinaya – mfano wa maneno, anawakusudia watu fulani wafanyao yanayofanana na yafanywayo na shetani:

"Angalia! Kwa hakika shetani amekusanya kundi lake, na amewaleta wapanda farasi wake na askari waendao kwa miguu. Nami nina busara yangu. Sijajidanganya wala sijadanganywa. Nitawajazia hodhi la maji ambalo mimi ndiye mfutaji wake, hawarudi baada ya kunywa wala hawatolirudia."1

---

1. Yaani hilo hodhi la maji ni mfano wa vita; hawarudi baada ya kunywa, yaani wakija kwenye mapambano hayo watakufa na hawatorudi walikotoka, na watakaonusurika na kifo hawatorudi tena kuchochea vita vingine.

11. Na Katika Maneno Yake (A.S)

Kwa mwanawe Muhammad ibnul–Hanafiyya alipokuwa akimpa bendera siku ya Jamal:

"Milima huenda ikaondoka na ikatoweka (mahali pake) wewe usiondoke! Uma meno yako.1 Mwazime Mungu fuvu lako la kichwa chako. Imarisha nyayo zako ardhini, mtazame adui wa mbali, fumba macho yako.2 (Yaani usiogope adui kwa kujali wingi wao na kutishika), jua kuwa ushindi ni kutoka mwa Mwenyezi Mungu swt.

---

1. Kauli yake: Uma meno yako, yasemekana mwenye kuuma meno yake mshale hauathiri ubongo wake, kwa sababu mifupa ya kichwa hukomaa na kuwa migumu. Na kauli yake: Air'llaha jum jumataka maana yake litumie hilo katika utii wa Mungu.
2. Tupa macho yako; yaani, zizunguke harakati zao zote, na yafumbie macho yale yanayokutisha kutokana nao, yaani lisikutishe la kutisha bali lifumbie macho.

12. Miongoni Mwa Maneno Yake (A.S)

Mwenyezi Mungu alipompa ushindi dhidi ya watu wa Jamal (Ngamia). Mmoja kati ya Sahaba wake alisema: "Natamani lau ndugu yangu fulani angekuwa yupo, ili aone ushindi Mungu aliokusaidia kuupata dhidi ya maadui zako." Hapo akasema (a.s):

"Je, mwelemeo na upendo wa ndugu yako u pamoja nasi?" Akasema: "Ndiyo," akasema (a.s): "Basi itakuwa kwamba alikuwa pamoja nasi katika kikosi cha askari wetu hawa, kwa hakika walikuwa wapo hata wale ambao bado wapo viunoni mwa wanaume na mifuko ya uzazi ya wanawake, punde tu wakati utawatoa, na kwa wao imani itakuwa na nguvu".

13. Na Miongoni Mwa Maneno Yake (A.S)

Kuwalaumu watu wa Basra baada ya vita vya Jamal (Ngamia):

Mlikuwa askari wa mwanamke, na wafuasi wa mnyama;[1] amepiga kelele mkamwitika, na akajeruhiwa mkakimbia. Tabia zenu ni mbaya na ahadi zenu ni khiyana na dini yenu ni unafiki, maji yenu ya chumvi.[2] Mwenye kuishi kati yenu yuko rehani kwa dhambi zake, mwenye kuondoka kwenu atapata amani ya rehema kutoka kwa Mola wake Mlezi. Kama nauona msikiti wenu wafanana na sehemu ya mbele ya Safina (boti), Mungu ameipeleka adhabu kutoka juu na kutoka chini yake, na waliomo humo wamezama."

Na katika riwaya nyingine: "Wallahi mji wenu utazama, kana kwamba nauona msikiti wenu ukiwa kama sehemu ya mbele ya boti au mbuni aliyeanguka kwa kifua chake."

Na katika usemi wake mwingine: "Kama kifua cha ndege katika kilindi cha bahari."

Na katika usemi wake mwingine: "Mji wenu ni miongoni mwa miji ya Mungu ambayo udongo wake unanuka sana, ukaribu mno na maji, na umbali mno na mbingu, na una sehemu tisa katika kumi ya maovu, aingiaye humo huzungukwa na dhambi zake na atokaye humo huneemeka na msamaha wa Mungu. Naona mji wenu kama kwamba umefunikwa na maji kiasi kwamba hakuna kinachoonekana isipokuwa sehemu ya juu ya msikiti, ukiwa kama kifua cha ndege katika kilindi cha bahari."

---

1. Atba'ul-bahima: Wafuasi wa mnyama, yaani ngamia, na ngamia wa Aisha alikuwa ni bendera ya kikosi cha Basra, waliuawa kwa ajili yake kama watu wanavyouliwa chini ya bendera yake.
2. Maji yenu ya chumvi, waweza kuduwaa vipi washutumiwe maji kuwa ya chumvi hiyo si miongoni mwa sifa za matendo

yao! Jibu: Hilo japo si katika matendo yao, ila ni mion– goni mwa lawama za mji. Kisha ameeleza mkazi wake ni mtu aliye rehani kwa dhambi yake, kwa kuwa yawezekana awe ashiriki nao katika dhambi au aiona dhambi yatendwa na hakanushi; Na madh'habu ya sahiba zetu ni kuwa haijuzu kuishi katika nchi ya kifasiqi, kama ambavyo haijuzu kuishi katika nchi ya kikafiri.

14. Na Miongoni Mwa Usemi Wake (A.S)

Katika mfano kama huo:

Ardhi yenu ipo karibu na maji. Iko mbali na mbingu.1 Akili zenu ziko nyepesi, pia zimejaa upuuzi. Kwa hiyo ninyi ni kilengwa cha mtupa mshale, na cha mlaji, na ni windo la mwindaji.

---

1. Karibu na maji: Yaani karibu na kuzama kwa maji na iko mbali na mbingu; kwa kuwa watu wa ilmu ya anga na wajishughulishao na sayari wanaeleza: (kuwa sehemu iliyo mbali zaidi na mbingu ardhini ni Ubla nayo ni sehemu karibu na Basra; na hilo linaafikiana na kauli yake (a.s). Na Basra ni mkoa katika nchi ya Iraqi na ndio mkoa wenye bandari.

15. Miongoni Mwa Maneno Yake (A.S)

Kuhusiana na ardhi alizozirudisha kwa Waislamu kutoka *Qata'iu* za Uthman: 1

"Wallahi hata ningezikuta (mali) zimetumika zikiwa mahari kwa kuolea wake, na vijakazi wamemilikiwa kwazo, ningezirudisha, kwa sababu kuwa katika uadilifu kuna wasaa.

Na ambaye umemuwia dhiki uadilifu, udhalimu kwake utakuwa dhiki mno.2

---

1. Qata'iu: Ni mali huikata Imam kuwapa baadhi ya raia kutoka ardhi ya Baitul'mali yenye kodi na huondoa kodi yake kisha anaifanya ilipiwe kiasi kidogo badala ya kodi. Na Uthman Affan aliwakatia ardhi nyingi Bani Umayah na watu wengine katika wapenzi wake na sahibu zake. Mfano wa kipande cha ardhi alichompa Mu'awiyah na Marwan. Na ilikuwa kwa kawaida mavuno yake hupewa wasafiri, na walio mfano wake.
2. Yaani ambaye atashindwa kupanga mambo yake kwa uadilifu hivyo yeye kuyapanga kwa udhalimu ni mwenye kushindwa zaidi, kwa sababu katika udhalimu kunadhaniwa kukabiliwa na upinzani na kuzuiwa. Na hotuba hii imeelezwa na al–Kalbiy yenyewe ni riwaya mar'fu'u – iliyorushiwa – kwa Abi Swaleh kutoka kwa ibn Abbas: Kuwa Ali alihutubia siku ya pili baada ya Ba'ia yake huko Madina; alisema: 'Alaa kila kipande alichokikata Uthman na kila mali ambayo amempa mtu kutoka kwenye mali ya Mungu itarejeshwa Ba'itul–Mal, kwa sababu haki ya zamani haibatilishwi na kitu, japo ningeikuta imetumika kwa kuolea...'

16. Miongoni Mwa Maneno Yake (A.S)

Baada ya kufanyiwa Bai'a huko Madina, na katika khutba hii anawa- pa watu habari juu ya ilimu yake ya yale yatakayojiri.

"Mimi ni dhamana wa niyasemayo, nayo yapo juu yangu. Kwa kweli mwenye kudhihirikiwa na mazingatio ya adhabu ya waliopita1 iliyoko mbele yake taqwa itamzuia kujiingiza kwenye mambo yanayoshukiwa. Juweni kuwa balaa lenu limerudi katika sura yake ilivyo kuwa siku ambayo Mungu alimtuma Nabii wake (s.a.w).2

Naapa kwa ambaye alimtuma (Muhammad {s.a.w}) kwa ukweli mtachanganyikiwa vikali kabisa, na kutikiswa sana, na mtapigwa mfano wa mpigo wa chungu3 mpaka aje juu aliyekuwa chini kati yenu, na aliyekuwa juu kati yenu aende chini, na Wallahi watatangulia waliokuwa nyuma, watachelewa nyuma waliokuwa wametangulia."4

"Wallahi sikuwahi kuficha neno,5 na mimi sikuwahi kusema uwongo na nilikwishapewa habari kuhusu hali hii na siku hii. Juweni kuwa makosa ni kama farasi aliyeasi (asiyepandika), wahusikao naye wamebebeshwa juu yake na akaondolewa hatamu zake na akawaingiza motoni.

Ala! Juweni kuwa taqwa ni mfano wa farasi aliyefundishwa, wamebebeshwa wahusikao naye juu yake na wakakabidhiwa hatamu yake na akawafikisha Peponi. Kuna haki na kuna batili, na kila moja ina watu wake, 6 endapo batili ikishika hatamu, na toka zamani imefanya hivyo,7 haki itaghilibiwa. Na haki inapokuwa ndogo, na imepata kuwa hivyo, ni mara chache kilichochelewa nyuma kuja mbele.8

Maelezo: Sayed Sharif alisema: kwa kweli ndani ya maneno haya machache kuna uzuri kuliko iwezavyo kutambuliwa, na kiwango cha kustaajabisha kilichochochewa nayo, ni zaidi kuliko utambuzi. Pamoja na hali tuliyoieleza muna ufasaha wa hali ya juu usiowezakufikiwa na mwingine. Na hawezi kuyatambua nisemayo isipokuwa mwenye kuwa na uelewa wa fani hii na kujuwa ilivyo. (Na hawaifahamu ila wenye ilimu; 29:43)

Na Miongoni Mwa Yaliyo Katika Khutba Hii

"Ameshughulishwa ambaye pepo na moto vi mbele yake! Mwenye juhudi na kuharakia atafaulu, na mtafutaji goigoi atakuwa na matumaini, mwenye kuzembea ataangamia motoni. Kulia na kushoto ni njia za upotofu, na njia ya kati ndio njia ya sawa, juu yake kuna Kitabu cha Milele na athari ya Nabii, na humo ndio mapitio ya Sunna na kwayo ndiyo hitimisho la matokeo."

Mwenye kudai kinyume ameangamia na mwenye kuzua amepata hasara. Mwenye kukengeuka kwa uso wake ameangamia. Na yatosha mtu kuwa mjinga kwa kutojua hadhi yake.

Hatoangamia aliyethibiti katika maoteo ya Uchamungu, wala mimea ya watu iliyo kwenye maoteo ya uchamungu haitokosa maji. Hivyo basi jisi– tirini majumbani mwenu, jirekibesheni wenyewe. Toba iko nyuma yenu, yampasa mtu kuhimidi asimhimidi ila Mola wake tu. Na mwenye kulaumu asilaumu ila nafsi yake.

---

1. Yaani mwenye kudhihirikiwa na uelewa wa hali ya waliopita kabla yake na akathibitiki– wa na mazingatio na kuonyeka kuwa adhabu iliowashukia watu wa Umma na vizazi na mtu mmoja mmoja kama kupatwa na unyonge, udhalili, ufakiri na hali mbaya atatambua kuwa yaliletwa na matendo yao ya dhulma, uadui na ujinga, waliojivika na kuharibika kwa hali, taqwa ambayo ni kujihifadhi asiingie kwenye mambo yaliyosababisha adhabu hizo kwa wahusika itamzuia asijiingize kwenye mambo yanayoshakiwa na kuporomokea humo. Kwa sababu mambo yanayo shakiwa ni dhana ya dhanio la makosa na makosa ndio yaletayo adhabu.
2. Balaa na tabu ya Waarabu iliokuwa imewazunguka siku ambayo Mungu (s.w.t) alimtuma Nabii wake Muhammad (s.a.w.w) ni balaa la mfarakano na shida ya mtawanyiko, kwa vile walikuwa wanabughudhiana wenye kuchukiana kila mmoja anashikilia upendeleo wa kabila, ukoo wake, na hunadi kwa moto au kaulimbiu ya ndugu zake wa karibu. Baadhi yao wanakata shingo za wanzao. Hiyo ndio hali iliyoangamiza umma mbali mbali. Sasa wamekuwa katika hali hiyo baada ya kuuliwa Uthman, hali ambayo imeleta uadui ambao dini ya Kiislamu ilikwisha uuwa, kukaibuka moyo wa uadui kati ya Bani Ummayah na Bani Hashim, na wafuasi wa kila upande, walaa haula walaquwata illa billahi.
3. Mpigo wa chungu: Yaani kama zinavyochanganyika, kokwa au nafaka, na mfano wake katika chungu; wakati wa kuchemka, ya juu huenda chini na ya chini huja juu, na huo ni mfano wa jinsi watakavyokuwa katika tofauti, na kutengana kwa udugu wa damu na kuharibika kwa nidhamu.
4. Kutangulia waliokuwa nyuma ni mfano wa Muawiyah kunyakua na kupanda kwenye jukwaa la Ukhalifa, hali ilikuwa hatazamiwi wala hakudhaniwa kuwa angelifikia Ukhalifa, na walichelewa watu wa nyumba ya Nabii kuufikia Ukhalifa hali walikuwa ndio wataraji– wa wa kwanza.
5. Alikuwa (a.s) hafichi kila kitu kinachompitia nafsini mwake, alikuwa muamrishaji wa mambo mema, na mkatazaji wa maovu, hapendelei, haendekezi mtu, hasemi uwongo. Na sehemu hii ni maandalizi ya usemi wake: “Nilikwishapewa habari kuhusu nafasi hii,” yaani alipewa habari na Nabii (s.a.w.w.) kuwa atakuwa katika hali hii na atajiwa na siku mfano wa siku hii.
6. Yaani: Jinsi mwanadamu ambavyo haepukani na mambo mawili, haki na batili, ulimwengu hauwi bila ya hayo mawili; Na kila moja kati ya mawili hayo lina watu wake, haki ina watu wake na batili ina watu wake.
7. Na endapo batili itakithiri kwa kukithiri wasaidizi wake, na hilo limekuwa toka hapo zamani kwa kuwa macho yaliyopotoka mbali na ukweli ni mengi kuliko yaliyothibiti juu ya ukweli. Japo ukweli uwe kidogo kwa uchache wa wasaidizi wake, huenda uchache wake ukashindwa na wingi wa batili na huenda batili ikazidi nguvu ukweli na kuutokomeza.
8. Neno hili, limekuja kutokana na kuchukizwa kwake (a.s.), hivyo, ameona ni vigumu kurejea dola ya kaumu baada ya kuwatoka, na kwenye maana hii amesema mshairi: “Wamesema, maji hurudi mtoni baada ya kunyauka mimea na kukauka mifereji. Nikasema; mpaka mto urejee kukimbia! na majani yaote pembezoni mwake! Wanakufa vyura.”

17. Miongoni Mwa Semi Wake (A.S.)

Maelezo kuhusu wanaotoa hukumu kati ya watu hali wakiwa hawastahiki: Pia katika usemi huo amewaainisha viumbe wenye kuchukiza mno kwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) wa aina mbili.

Aina ya kwanza: “Kwa kweli viumbe wenye kuchukiza sana mbele ya Mwenyezi Mungu ni watu (aina) wawili: Mtu ambaye Mungu (s.w.t) amemtelekeza yeye na nafsi yake. Huyu amepotoka mbali na njia ya kweli, 1anapenda sana kusema maneno ya bida’a na kuwaitia kwenye upotovu, kwa hiyo huyu ni fitna kwa wenye kudanganyika naye. Amepotea mbali na mwongozo wa waliokuwa wa kabla yake. Mwenye kuwapotosha wamfuatao maishani mwake na baada ya kufa kwake, mwenye kubeba makosa ya wengine, amekuwa rehani wa makosa yake.

Aina ya pili: “Mtu aliyekusanya ujinga, yu aharakisha kati ya umma wak– ijahili kuwaghushi na kuwadanganya. Haraka haraka afaidika na giza la fitna. Haoni faida iliyo katika utulivu. Walio mfano wa watu wamemwita mjuzi wala hayuko hivyo. Amefanya juhudi mapema asubuhi, na amekithirisha kukusanya vitu ambavyo uchache wake ni bora kuliko wingi wake, mpaka aondoapo kiu kwa maji machafu, na kukithirisha yasiyokuwa na maana, akaketi kati ya watu kama hakimu akichukua jukumu la kutatua yaliyowatatiza watu wengine, na endapo atafikwa na suala lenye maana isiyo dhahiri; ataliongelea kwa maneno mengi yasiyo kuwa na maana na kwa rai yake chakavu, kisha atalitolea maamuzi, kwa hiyo yeye katika kupanga mambo yenye utata ni kama utando wa buibui, hatambui amefanya sawa au amekosea; akifanya sawa yuahofia huenda amekosea, na akikosea huwa na matumaini ya kuwa amefanya sawa. Yu mjinga, anatangatanga bila ya mwongozo, haoni vizuri, mwenye kuyazamia mambo bila ya mwongozo.

Hakuishika ilimu kwa jino lenye makali. Riwaya anazipeperusha kama upepo upeperushavyo majani makavu.2

Wallahi hawezi kuyatatua vyema matatizo yaliyoletwa kwake, wala hafai kwa jukumu alilopewa.

Hajali kutojuwa asiyoyajuwa. Hatambui kuwa asilolijua yeye kuna ambao wanalijua. Na jambo lisipokuwa wazi kwake hulificha, kwa kuwa anajua kuwa mwenyewe ni mjinga. Damu zapiga kelele kutokana na hukumu zake zisizo za uadilifu, na mali zilizorithishwa vibaya zinamnung’unikia.

Ninalalamika kwa Mungu (s.w.t) kuwahusu watu wanaoishi ujingani na wanakufa katika hali ya upotovu, kwao wao hakuna kisicho na thamani zaidi kuliko Kitabu (Qur’ani) endapo kitasomwa ipasavyo,3 na wala hapana biashara yenye thamani zaidi kwa mauzo kuliko Kitabu (Qur’ani) endapo kitapotoshwa mbali na maeneo yake.

Wala hapana kiovu zaidi kwao kuliko mema, na hapana mema zaidi kuliko maovu!”

---

1. Al–Jai’ru: Mwenye kupotoka mbali na njia, na hiyo ni kinaya cha kwenda kwake nyuma ya nafsi yake katika itikadi yake, harejei kwenye ukweli wa dini, wala haongoki kwa dalili kutoka kitabuni, huyu ndiye aliyepotoka mbali na njia ya sawa, na amekwenda kombo.

2. Na katika riwaya nyingine: yadh’ruu riwayati kamaa tadhru riihul’hashiima, nayo ndiyo fasaha, Mwenyezi Mungu (s.w.t) amesema: (Fa asbah hashiiman tadhruuhur– riyaahu): – (mimea) ikawa vibua vinavyo peperushwa na upepo; 18:45). Hivyo basi, kama ulivyo upepo haujali katika kubeba majani makavu na kuyaparaganya, haujali kwa kuy– achanachana na

kutawanyika mpango wake, vivyo hivyo kwa huyu jahili huzifanyia riwaya kama upepo ufanyavyo kwa majani makavu.
3. Tuliya haqa tilawatihi: Ikisomwa ipasavyo; yaani ikichukuliwa kama inavyobidi na kama jumla zake zinavyojulisha, na ikafahamika kama alivyokuwa anaifahamu Nabii (s.a.w.w.) na masahaba zake walivyokuwa wanaifahamu.

18. Na Miongoni Mwa Maneno Yake (A.S)

Katika kulaumu tofauti za wanachuoni kwenye utoaji fatwa:
“Lamfikia mmojawao suala kuhusu hukumu mojawapo miongoni mwa hukumu, yeye analitolea hukumu kwa rai yake, kisha lamfikia tatizo lile lile mwanachuoni mwingine, yeye naye hulitolea hukumu tofauti na yule wa kwanza, kisha huwa makadhi au mahakimu wanakusanyika kwa

Khalifa aliyewatawaza ukadhi na hukumu zile, naye anazipitisha kuwa ziko sahihi rai zao zote, hali Mungu wao ni mmoja! Nabii wao ni mmoja! na Kitabu chao ni kimoja! Je Mungu (s.w.t) aliwaamuru watofautiane na wao wakamtii!? Au aliwakataza kutofautiana wakamuasi! Au Mungu (s.w.t) aliteremsha dini yenye upungufu akaomba msaada kwao ili kuikamilisha!? Au walikuwa washirika Wake, kwa hiyo wao waseme watakalo na Yeye (s.w.t) apaswe kuridhika!?

Au Mungu (s.w.t) aliteremsha dini iliyo kamili na Mtume (s.a.w.w.) alizembea kuifikisha na kuitekeleza!, hali Mungu (s.w.t) anasema: “Hatujapuuza kitabuni kitu chochote” (6:38) “Ndani yake muna ubainifu wa kila kitu” na amesema kuwa Kitabu baadhi yake kinaisadikisha baadhi nyingine na yakuwa hakuna hitilafu humo kama alivyosema (s.w.t): “Lau ingekuwa imetoka kwa asiye Mwenyezi Mungu, bila shaka wangelikuta ndani yake khitilafu nyingi”. (An-Nisaa:82). Na yakuwa Qur’ani dhahiri yake nzuri yastaajabisha na sehemu yake ya ndani imekwenda kwa kina sana. Maajabu yake hayaishi wala mageni yake hayamaliziki wala mafum- bo yake hayatofumbuliwa isipokuwa kwayo.

19. Miongoni Mwa Semi Zake (A.S)

Alimwambia Al-Ash’ath bin Qays, naye (a.s) akiwa juu ya mimbari ya al-Kufa akitoa hutba, kulipita jambo katika baadhi ya usemi wake ambalo Al-Ash’ath alilipinga. Akasema al-Ash’ath: “Yaa Amiral-Mu’minin, hili liko dhidi yako haliko kwa upande wako.”1 Aliinamisha macho yake (a.s) na kutikisa kichwa na kumwangalia, kisha akasema:

“Ni jambo gani linalokujulisha lililo dhidi yangu na ambalo ni langu! Laana ya Mungu iwe juu yako, na laana ya wenye kulaani, umfumaji, mtoto wa mfumaji,2 wewe ni mnafiki mtoto wa kafiri. Wallahi ukafiri ulikuteka mara moja na uislamu mara nyingine.3 Hukufidiwa kutoka mojawapo, si kwa mali yako wala

kwa ukoo wako.

Mtu huyu aliwafanyia hila watu wake wakapigwa kwa upanga na aliwasukumia kifo na maangamizi, anastahili kuchukiwa na watu wa karibu na haaminiwi na watu wa mbali.

Maelezo: ar-Radhiyu (r.a.) amesema: "Amirul-Mu'minin (a.s) anakusudia kwamba huyu Ash'ath alitekwa akiwa mfungwa wa vita katika vita zama za ukafiri mara moja na katika Uislamu mara moja. Ama usemi wake (a.s.): (*Dalla alaa Qaumihi saifa*) alikusudia tukio lilikuwa kati ya Ash'ath na Khalid bin Al'Waliid huko Yamamah, aliwaghuri watu wake na kuwafanyia hila mpaka akasababisha Khalid awapige vita kwa upanga. Na baada ya hapo watu wa kaumu yake walikuwa wanamwita: "***urfu nnari***" nalo ni jina la mtu mdanganyifu kwao."

---

1. Amirul-Mu'minin alikuwa anazungumzia kuhusu suala la mahakimu wawili, mtu mmoja katika sahaba zake alisimama akasema: "Ulitukataza kupitisha hukumu, kisha ulituamrisha tufanye hukumu, hivyo hatujui ipi kati ya amri mbili hizi yenye mwongozo kwa kuilinganisha na nyingine!" Yeye (a.s.) akapiga mkono wake juu ya mwingine na akasema: "Haya ni malipo ya mwenye kuacha itikadi." Hapo ndipo al-Ash'ath alisema alilosema, na Amirul-Mu'minin anakusudia kuwa: Haya ndiyo malipo yenu kwa vile muliacha uthabiti na kufanya ghasia na mukanifanya nilazimike kukubali maamuzi yenu.
2. Mfumaji: Na yasemekana kuwa wafumaji wanajulikana kwa upungufu wa akili sana katika watu, na Wayemeni huaibishwa kwa kuitwa wafumaji. Na Ash'ath ni mtu wa Yemen kutoka kijiji cha Kinda. Ash'ath alikuwa katika Sahaba wa Imam Ali (a.s) kama alivyokuwa Abdullah bin Ubayy bin Salul katika maswahaba wa Mtume wa Mungu (s.a.w.w), kila mmoja kati ya hawa wawili ni kiini cha unafiki katika zama zake.
3. Ametekwa mara mbili: Mara akiwa kafiri katika baadhi ya vita vya kijahiliya, na hivyo ilikuwa kabila la Muradi lilimuua Qais al-Ashaji, baba wa Ash'ath, yeye al-Ash'ath alitoka ili kulipiza kisasi cha baba yake.

20. Katika Usemi Wake (A.S.)

Katika kukhofisha juu ya hali ya mambo itakavyokuwa baada ya mauti:
"Kwa hakika ninyi lau mungeyaona waliyoyaona waliokufa katika ninyi, mngefadhaishwa na kutishika, na mngesikiliza na kutii. Lakini yamefichika kwenu yale waliyoyaona, hivi punde pazia litaondolewa.1

Mmeoneshwa isipokuwa kama hamkuona, na mmesikilizishwa, isipokuwa kama hamkusikia, na mumeongozwa isipokuwa kama hamkuongoka. Kwa haki nakuambieni mazingatio yamekudhihirikieni, na mumeonywa na ambayo (mtu) anaweza kuonyeka. Baada ya wajumbe wa mbingu (malaika) ni mwanadamu tu ndiye awezaye kufikisha ujumbe kutoka kwa Mungu.2

---

1. Hivi punde pazia litaondolewa, na hilo litakuwa mwisho wa umri, na mtu kufika nyumba ya kwanza miongoni mwa nyumba za akhera, na maneno haya yanajulisha usahihi wa kauli ya adhabu ya kaburi.

2. Wajumbe wa mbinguni: Malaika, yaani endapo mutasema hakijatujia kitu kutoka kwa Mungu; jibu ni, hoja imesimamishwa dhidi yenu kwa tablighi ya Mtume wa Mungu na mwongozo wa khalifa wake. Yashabihiana na kauli yake (a.s.): "Lau mungeyaona bayana waliyoyaona waliokufa kabla yenu." Na kauli ya Abu Haazim akimwambia Sulaiman bin Abdil'Maliki katika maneno aliyokuwa anamuwaidhi nayo: "Kwa hakika baba zako wamelifanya suala hili ovyo ovyo bila ya ushauri, kisha wamekufa, lau ungejua waliyosema na waliyoambiwa!" Imeelezwa kuwa: "Alilia mpaka alianguka."

21. Na Katika Jumla Ya Semi Zake (A.S.)

Ili kuwawaidhi watu:-

"Kwa kweli lengo liko mbele yenu.1 Na kwa kweli nyuma yenu kuna (saa) kiyama kinakupelekeni munakoelekea. Jifanyeni wepesi mutawakuta,2 bali tu, wa kwanza wenu wanawangoja wa mwisho wenu."3

Maelezo: Sharif Ar-Radii (r.a) alisema: "Nasema kwa kweli maneno haya ya Ali lau yangewekwa kwenye mizani upande mmoja na maneno mengine upande mwingine mbali na maneno ya Mungu na maneno ya Mtume wake Mizani ingekuja chini kwa uzito wa maneno ya Ali, na yangethibiti kuwa na ushindi katika nyanja zote. Na usemi wake: "*Takhaffafu tal'haqu*" Kuweni wepesi mtashinda' ni ibara fupi sana kupata kusikika iliyo na maana kubwa mno! Ina maana pana iliyoje! Bubujiko la hikima. Tumeishiria ukubwa wa maana yake katika Kitabu "*Al-Khasa'is*."

---

1. Lengo la mukalafiina: Imma ni matokeo ya malipo mema, au adhabu, kwa hiyo inawezekana iwe alikusudia hilo, na inawezekana iwe alikusudia kwa neno lengo - umauti, ila tu amejaalia hilo mbele yetu; kwa sababu mwanadamu ni kama mwenye kwenda kuuelekea umauti, au anakwenda kuyaelekea malipo, hivyo basi hayo mawili yako mbele yake.
2. Takhaffafu talhaqu: Asili yake, mtu anakwenda mbio naye hana uzito wa akibebacho, anastahili kuwakuta waliomtangulia, na wametangulia waliotangulia na matendo yao kwenye wema, basi mwenye kutaka kuwakuta ni juu yake ajifanye mwepesi mbali na uzito wa matamanio, na mzigo wa taabu katika kuzipata ladha, na akimbie binafsi mbali na haya yanayoisha, hivyo basi atawakuta ambao waliofuzu kwa nyumba ya baadae.
3. Yaani waliotangulia kufa hawatofufuka, watafanywa wangojee mpaka watakapofika waliobaki hai, wote na iishe duru ya mwanadamu hapa duniani. Wala hatobaki juu ya uso ya ardhi yeyote, hapo ndio sasa itakuwa imewadia, nayo ndio siku watafufuka.

22. Miongoni Mwa Khutba Zake (A.S)

Walipomtuhumu kumuuwa Uthman (r.a):

“Jihadhari! Kwa kweli shetani ameanza kuwahimiza watu wake, na amekusanya wenzake ili udhalimu urejee kwenye nafasi yake, na irejee batili kwenye kiwango chake. Wallahi hawajaniona na jambo ovu waka- likanusha, wala hawajafanya insafu kati yangu na wao.

Kwa kweli wao wanaidai haki ambayo wameitelekeza, na damu ambayo wameimwaga, ikiwa nilikuwa mshirika wao basi bila shaka wana hisa humo, na ikiwa wao ndio waliotenda bila ya mimi, kisasi kitakuwa juu yao tu. Kwa kweli hoja yao kubwa dhidi yangu iko dhidi yao wenyewe.

Wananyonyesha kwa mama alieacha kunyonyesha. Wanaihuisha bidaa iliyokwishauawa.
Oh! wee mdai usiyefanikiwa, njoo! Huu ndio wakati wako.[1] Nani mdai? Na kwa lipi ameitikiwa? Mimi naridhika na hoja ya Mungu dhidi yao na ujuzi Wake kwao.”

Tishio la Vita!

“Endapo watakataa nitawakabili kwa makali ya upanga, ambao ni mponya- ji wa matendo batili na ni mnusuru wa haki. Yashangaza eti wamenitumia khabari ya kuwa nitoke kujiandaa na mapambano ya kuchomana mikuki na niwe tayari kwa vita vya upanga! Akina mama waombolezaji wawalilie. Nilikuwa na ningali sihofishwi na vita wala kutishika na kupigwa. Nina yakini kwa Mola Wangu Mlezi na sina shaka na dini yangu”.

---

1. Mdai: Ni mmoja katika watatu: wanaume wawili na mwanamke, ambao wametajwa katika kisa cha ngamia. (Man da'a waila madha ujiiba!? - Yaani ni kama kusema; Wadharauni watu walioitwa na mwitaji huyu! na liangalieni suala hili waliloitika wito kwa ajili yake kuwa ni baya mno.

23. Miongoni Mwa Khutba Zake (A.S)

Kuhusu mgao wa riziki:

“Hivyo, kwa kweli amri yateremka kutoka mbinguni mpaka ardhini kama matone ya mvua na kuifikia kila nafsi kiwango ilichogawiwa, ikiwa ni zaidi au pungufu, kwa hiyo endapo mmoja wenu anapoona kwa nduguye wingi wa ahli au mali au binafsi hilo lisimkere, kwa kuwa Muislamu hatendi kitendo ambacho lau kitafichuka atainamisha macho yake (kuona haya) na ambacho watu wasio na mashiko watashawishika, yeye ni mfano wa mcheza kamari anayetumainia mchezo wake wa kwanza utamhakikishia kipato na yakuwa utamfidia michezo ya nyuma aliyopata hasara.

Ni sawa na Mwislamu asiye na hiyana, anatazamia kwa Mungu mojawapo ya mazuri mawili: Ima wito kutoka kwa Mwenyezi Mungu, na yaliyo kwa Mungu ni bora kwake. Au riziki ya Mungu, tayari ana

watoto na mali, pia atakuwa na dini yake na hishma yake.

Na kweli mali na watoto ni matunda ya dunia tu, na matendo mema ni matunda ya akhera. Na Mungu (s.w.t) huenda akayakusanya mawili hayo kwa baadhi ya kaumu ya watu.

Jihadharini na yale Mungu Aliyo wahadharisheni, na mwogopeni kwa kiasi kwamba haitohitajika kuomba msamaha. Na fanyeni (wema) bila ya kutaka kujionesha au kusikika, kwa kuwa atendaye kwa ajili ya mwingine ambaye si Mungu, Mungu atamuwakilisha kwa yule aliyetenda kwa ajili yake.

Tunamuomba Mungu (s.w.t) mafikio ya mashahidi na tuishi maisha ya walio na maisha ya furaha, na kuwa pamoja na manabii.

Oh ninyi watu! mtu hawezi kujitosha – japo awe na mali – bila ya jamaa wa ukoo wake, na ulinzi wao juu yake kwa mikono yao na ndimi zao. Nao ni watu muhimu sana kwa uangalizi nyuma yake, nao ni kiunganishi mno cha mfarakano na ndugu zake, ni wenye huruma mno kwake anapokumbwa na shida. Utajo mwema Mungu amjaaliao mtu miongoni mwa watu ni bora kwake kuliko mali ambayo atawarithisha watu wengine".

Utajo mwema kwa haki: Nao kwa ndugu ni bora na ni laiki yake:

Na miongoni mwa sehemu ya khutba hii: "Ala! Mtu asiache kusaidia haja aionayo kwa ndugu wa karibu, awaonapo katika shida azitatue, kwa kile ambacho hakitomzidishia au kumsaidia chochote akiacha, na wala hakitompunguzia chochote endapo atakitumia.

Na ambaye anauzuia mkono wake kuwasaidia ndugu zake wa karibu, ukweli ni kwamba unazuilika kutoka kwake kuwaendea wao mkono mmoja tu, na itazuilika kwake kutoka kwao mikono mingi. Mwenye tabia nzuri, mapenzi yake kwa ndugu yatadumu.

Maelezo: Amesema Sharif ar-Raadhiy; "Nasema *Alghafiratu* hapa ina maana ya kuzidi na uwingi, kutokana na usemi wao (Waarabu) kuhusu kundi la watu" *Aljammau Alghafiru*, yaani kundi kubwa la watu, na *Aljam'u-Alghafiiru*, ikiwa na maana hiyo hiyo. Na yaelezwa (*If 'watun min Ahlin au mali*) na *Al'If 'watu*; ni kitu bora, husema; *Akaltu af 'wata ta'ami* – nimekula chakula kilicho bora. Maana nzuri iliyoje aliyoikusudia (amani imfikie) kwa usemi wake mwenye kuuzuia mkono wake kwa kutowasaidia jamaa zake... mpaka mwisho wa usemi wake huo, kwa kweli mzuiaji kwa nduguye anazuia manufaa ya kheri ya mkono mmoja. Naye atakapohitaji nusura yao, na atakapodharurika na usaidizi wao, wao wata- jizuia kumnusuru, na watakuwa wazito kumpa sauti, kwa hiyo itakuwa umezuilika msaada wa mikono mingi, na kusimama nyayo nyingi.

24. Na Miongoni Mwa Khutba Zake (A.S)

Katika kuhimiza kuwapiga vita Khawarij:

“Naapa kwa umri wangu siko legelege wala dhaifu katika kupigana na mwenye kuhalifu ukweli na kuyumbayumba ndani ya upotovu. Hivyo basi waja wa Mungu mcheni Mungu kimbilieni kwa Mungu kutoka kwa Mungu.1

Nendeni katika njia ya wazi aliyokufanyieni. Tekelezeni yale aliyowaambatanisha nayo. Kwa kuwa Ali ni mwenye kuchukua dhamana ya kufuzu kwenu hapo baadaye endapo hamtatunukiwa hivi punde.

---

1. Kimbieni kutoka kwa Mungu kwenda kwa Mungu: Yaani, kimbieni kuielekea rehema ya Mungu kutoka adhabu yake.

25. Na Miongoni Mwa Khutba Zake (A.S)

Habari zimeenea na kumfikia kuwa watu wa Muawiyah wameteka nchi (Yemen) na wafanyakazi wake wawili wa Yemen walimjia, nao ni Ubaidullahi bin Abbas na Saeed bin Namran alipowashinda nguvu Busru bin Abii Artaat. Hapo (amani imfikie), alisimama juu ya mimbari akiwa ameudhika na watu wake kuwa wazito kwenye jihadi na kuwa kwao kinyume na yeye katika rai, akasema:

“Hakuna kilichobakia isipokuwa (mji wa) Kufah, naweza kuukunja na kuukunjua,1 kama haukuwa ila ni wewe2 kimbunga chako kinavuma Mungu akuweke katika hali mbaya!”

Alitolea mfano ubeti wa shairi:

Oh! ewe Amr uzuri wa maisha mema ya babako,
Nimeambulia makombo kidogo mchuzi wa kile chombo.

Hatimaye alisema (a.s):

“Nimepata habari kuwa Busra amehujumu na kuitwaa Yemen, nami namuapa Mungu nina yakini watu hawa watawashindeni na watakuwa na dola juu yenu kwa sababu ya kushikamana katika batili yao, na kwa sababu ya kufarikiana kwenu katika haki yenu, na kwa kumuasi kwenu Imam wenu akiwa katika haki, na kwa kumtii kiongozi wao akiwa katika batili, na kwa kutekeleza amana kwa kiongozi wao na kwa hiyana yenu, na kuwa kwao wema katika nchi yao, na kwa kuwa kwenu waovu.

Kama mmoja wenu ningemwamini na bilauri ya kunywea maji, ningeogopa huenda akaondoka na mkono wake. Oh! ewe Allah, kwa kweli wamenichafua moyo na nimewachafu mioyo, nimewachoka nao wamenichoka.
Basi nibadilishie walio bora kuliko wao nami nibadilishe kwao na mwingine ambaye ni mshari zaidi kuliko mimi!
Oh! ewe Allah, ziyayushe nyoyo zao kama iyayukavyo chumvi ndani ya maji. Wallahi natamani lau ningekuwa na askari wapanda farasi elfu moja kutoka kwa Bani Firasi ibni Ghanmin kama asemavyo mshairi:

Lau utawaita watakujia miongoni mwao
Wapanda farasi kama wingu la kiangazi".

Kisha aliteremka kutoka mimbari. Ar-Radhwiyu amesema: "Nasema *Al'armiyatu* ni wingi wa neno *Ramiy*, ni mawingu. Na *Hamimu* hapa: ni wakati wa kiangazi. Na mshairi ameyataja khususan mawingu ya wakati wa kiangazi, kwa sababu yanakwenda haraka mno kwa kuwa hayana maji, na mawingu huenda kwa uzito kwa kujawa na maji. Hali hiyo haiwi aghalabu ila wakati wa masika. Na mshairi alikusudia kuwasifu kuja kwao haraka waitwapo na kutoa msaada waombwapo msaada. Na dalili ni usemi wake: ***hunalika lau daauta ataaka min hum*** - hapo endapo utawaita watakujia miongoni mwao."

---

1. Aqbidhuha wa absutuha: Yaani, nafanya humo kama afanyavyo mwenye nguo katika nguo yake, anaikunja na kuikunjua.
2. (Fa inlam takuni .....): Yaani, kama sina ninachomiliki katika dunia ila mji wa Kufah wenye fitna, ewe Allah itolee mbali!

26. Miongoni Mwa Khutba Zake (A.S)

Katika kuwalaumu waliomfanyia bai'a kwa sharti:

"Kwa kweli Mungu (s.w.t) alimtuma Muhammad (s.a.w.w) akiwa muonyaji kwa walimwengu na mwaminifu wa uteremsho (Qur'ani) na ninyi Waarabu mkiwa wafuasi wa dini ovu mno, na mkiwa mukiishi katika nchi yenye maisha magumu mno, kwenye mawe ya kwaruzayo na nyoka wenye sumu, mlikuwa mkinywa maji machafu sana na mnakula chakula cha ovyoovyo, mlikuwa mkimwaga damu zenu, mnakata mawasiliano na jamaa zenu. Sanamu zimesimamishwa mbele yenu, na dhambi zimekuambateni."

Na sehemu nyingine ya khutba hii:

"Niliangalia na kuona sina msaidizi isipokuwa watu wa nyumba yangu, hivyo nilijiepusha kuwatumbukiza

kwenye mauti, nilifumba macho yakiwa na chembe ya vumbi,1 na nilikunywa hali ya kwamba kooni kuna kilichokwama,2 na nilivuta subira katika kuvuta pumzi, na kwa uchungu mno kuliko ladha ya shubiri.”

Na sehemu ya khutba hii:

“Hakufanya baia3 hivyo basi haukufanikiwa mkono wa muuzaji na kutwezwa uaminifu wa mnunuzi,4 hivyo basi kuweni tayari kwa vita na mtayarishe zana zake, mwale wake umepanda na mwanga wake umepaa na mjiambatanishe na subira, kwa kuwa subira yaita kuelekea ushindi”.

---

1. Na shajaa ni kitu kilichonasa kooni uwe mfupa wa samaki au mfano anaupiga Amirul Muuminina hali ya mambo ilivyomuiya ngumu mfano wa afumbuaye macho yake yakiwa yamejaa uchafu.
2. Na amezaye sawa iwe maji au mfano wake akiwa na kilichomkwama kooni hiyo ndiyo hali iliyo mkabili Ali bin Abi Talib zama za ukhalifa wake.
3. Asiyefanya bai’a hapa ni Amr bin Al–Aas mpaka alipoweka sharti apewe thamani ya baia yake. Amru bin Al–Aas alimwambia Muawiyah kuwa atamfanyia bai'a endapo atakubali kumpa uliwali wa Misri endapo mambo yatamnyookea.
4. Mkono wa muuzaji ni Muawiyah bin Abii Sufiani, na ulitwezwa uaminifu wa mnunuzi! (yaani Amru bin al’Aas).

27. Miongoni Mwa Khutba Zake (A.S)

Katika kuhimiza jihadi na kuwalaumu wanao kaa nyuma:

“Kwa hiyo kwa kweli jihadi ni mlango katika jumla ya milango ya *Jannah* (peponi), Mwenyezi Mungu ameufunguwa kwa ajili ya wapenzi Wake makhsusi. Nayo ndio vazi la taqwa (uchamungu), na ni ngao ya Mungu yenye kuhifadhi, na stara yake thabiti.

Hivyo basi, mwenye kuiacha kwa kutoipenda, Mungu atamvisha nguo ya udhalili na balaa litamuenea na atadhalilishwa kwa kutwezwa, na kudharaulika, na moyoni mwake kuondolewa akili na fahamu. Ukweli umeondolewa kutoka kwake kwa sababu ya kuipoteza jihadi. Atakumbwa na aibu na kunyimwa insafu.1

Angalieni mimi nimekuwa nikikuiteni kupambana na watu hawa usiku na mchana, kwa siri na kwa tangazo la wazi, na nilikuambieni (washambulieni kabla hawajakushambulieni, wallahi watu hawajapata kushambuliwa katu katika kitovu cha nyumba yao ila watadhalilishwa) mkategeana na mkadhoofu, mpaka mliposhambuliwa na miji yenu ikatekwa; basi huyu nduguye Ghamid farasi wake wameingia Anbaar,2 na amemuua Hasan bin Hasan Al’Bakriy, na wamewaondoa farasi wenu kwenye ngome yao.

Na habari zimenifikia kuwa mtu miongoni mwao huingia kwa mwanamke Mwislamu na mwanamke dhimiy na anampora pambo la mguuni, bangili, kidani chake, na shanga na huwezi kumziwia ila kwa

kusema; (***Innaa lil lahi wain naa ilayhi raajiuna 2:156***) na istir'haam – kupiga kelele ili kuomba rehema kisha wakaondoka bila ya kupunguwa mtu kati yao. Hakupata mtu kati yao jeraha, wala kumwagika damu yao; lau mtu Mwislamu akifa baada ya hali hii, majonzini hangepaswa kulaumiwa, bali kwa mtazamo wangu angekuwa amestahiki!

Oh! Ajabu ilioje inavunja moyo na inahuzunisha, kuona hawa watu walivyokuwa na mshikamano katika matendo yao batili, na kusambaratika kwenu mbali na haki yenu! Ubaya na huzuni ilikufikeni, mlipokuwa lengo la kutupiwa mishale. Mnashambuliwa wala hamshambulii, mnahujumiwa wala hamhujumu. Mungu anafanyiwa maasi mmebaki mmeridhika.

Nikiwaamuruni kuwaendea siku za joto mnasema hili ni joto kali, tungojee joto lipungue, na nikikuamuruni kuwaendea wakati wa baridi mnasema hii ni baridi kali, tungojee baridi iondoke. Hivyo yote ni kukimbia joto na baridi; na mkiwa mwalikimbia joto na baridi, basi ninyi wallahi upanga mtakuwa ni wenye kuukimbia zaidi!"

Oh! Enyi mlio mfano wa wanaume wala si wanaume, fikra za kitoto, na mna akili mfano wa akili za wanawake watunza "nyumba ya mapambo." Natamani nisingewaona wala nisingewatambua kabisa – wallahi kuwajua huku kumeleta aibu na kumalizikia huzuni na hasara. Mungu awalaani, mmeujaza moyo wangu usaha na kuusheheni hasira, na mmeninywesha konga la huzuni konga baada ya konga, mmeichafua rai yangu kwa kuasi na kunitelekeza, kiasi cha kufikia makuraishi kusema; 'hakika mwana wa Abi Talib ni mtu shujaa lakini hana maarifa ya vita'

Mungu awahurumie, hivi kuna yeyote miongoni mwao mkali na mwenye uzoefu zaidi na wa tangu zaidi kuliko mimi. Nimeinukia nayo nikiwa sijafikia umri wa miaka ishirini, na bado, mimi huyo niko humo nikiwa nimevuka miaka sitini, lakini hana rai muwafaka asiyetiiwa!"

---

1. Insafu ni uadilifu; atanyimwa uadilifu kwa kuwa Mungu atajaalia mtu atakayemzidi nguvu na kumdhulumu haki yake.
2. Anbaar: Ni mji ulioko ukingo wa mashariki wa mto wa Furati.

28. Na Miongoni Mwa Khutba Zake (A.S)

Katika kuhamasisha maandalizi ya masurufu ya akhera:

"Hivyo sasa kwa kweli dunia imetupa mgongo na kutangaza msafara kuaga kwake. Na kwa kweli akhera imewadia na kupiga mbiu ya kuja kwake ghafla.

Lo! Kwa kweli leo ni siku hasa ya maandalizi, na kesho ndio mashindano ya mbio, na nishani ni

(Jannah) Pepo, na mwisho wake ni moto; je hakuna mwenye kutubu kwa makosa yake kabla ya mauti yake? Je hakuna wakutenda mema kwa ajili yake kabla ya siku atakayokuwa na haja kubwa. Angalia! ninyi mpo katika siku za matumaini, ambazo nyuma yake kuna mauti.

Hivyo mwenye kutenda mema katika siku zake za matumaini kabla ya kufikiwa na ajali yake, atakuwa amenufaishwa na matendo yake, na kifo chake hakitomdhuru, na mwenye kufanya uzembe katika siku zake za matumaini kabla ya kufikiwa na ajali yake, atakuwa amepata hasara kazi yake, na ajali yake itamdhuru. Angalia! fanyeni wema wakati wa upendo wenu kama mfanyavyo wakati wa hofu.

Angalia! kwa hakika mimi sijaona kilichotelekezwa kama *jannah* (Pepo) kwani amelala mwenye kuitafuta, wala kuona kitu kilichopuuzwa kama moto amelala aukimbiaye.1

Angalia, asiyenufaika na ukweli bila shaka batili itamdhuru,2 na ambaye hawi mnyofu kwa mwongozo, upotovu utamkokota na kumzamisha kwenye maangamizi.

Alaa! kwa kweli ninyi mmeamriwa kufanya msafara,3 na mmeoneshwa masurufu; na kwa kweli ninalohofia mno kwenu ni kufuata utashi mbaya wa nafsi na kurefusha matumanini, basi chukueni masurufu kutoka hapa duniani ambayo kwayo mutakayojihifadhi nayo kesho nafsi zenu".

Maelezo: Sharifu Ar-Radhiy (r.a) amesema; (Nasema): Kuwa lau kungekuwa kuna maneno yawezayo kumshika mtu shingo na kumfanya aipige pande dunia na kulazimika kutenda mema kwa ajili ya akhera, yangekuwa maneno haya. Na yanatosha kuwa yenye kukata viambatisho vya matumaini (makubwa ya kubaki duniani). Na ni yenye kuwasha msukumo wa kuonyeka na kujikataza.

Na la kustaajabisha mno ni usemi wake (a.s) Alaa! Leo ni siku ya maandalizi, na kesho ndio mashindano ya mbio, na nishani itakuwa pepo na mwisho wake ni moto. Kwa kuwa humo, pamoja na utukufu wa tamko, na adhama ya thamani ya maana, na ukweli wa mithali na uhakika wa tash'biihi, kuna siri ya kustaajabisha, na maana nzuri.

Nayo ni ile kauli yake (a.s): *WA SABAQATU AL JANNATU WAL GHAAYATU ANNARU,* akatofautisha kati ya matamko mawili kwa sababu ya kutofautiana maana mbili, wala hakusema; *WASABAQATU ANNARU WALGHAAYATUL JANNAH kama* alivyosema; *ASSABAQATU AL-JANNATU,* kwa sababu (al-Istibaq - kushindana) huwa kwenye jambo lipendwalo na lengo litakiwalo. Na hiyo ni sifa ya Jannah, wala maana hii haipo katika moto.

Tunajilinda kwa Mungu tuwe mbali nao, kwa hiyo haikufaa aseme: *WASABAQATU ANNARU* bali amesema; *WALGHAAYATU ANNARU* kwa kuwa *ALGHAYA* ni mwisho wa jambo, au matokeo yake, kwani mwisho huwa kwa aupendaye na asiyeupenda kwa hiyo ndiyo maana ikawa yafaa alitumiye neno hilo kwa ajili ya mambo mawili yote. Kwa hiyo neno hilo mahali hapa ni kama matokeo na mwisho wa jambo.

Mungu (s.w.t) amesema; *QUL: TAMATA'U FA INNA MASWIRAKUM ILANNARI* - **sema: Stareheni!**

Kwani marejeo yenu ni motoni; 14:30). Wala haifai mahali hapa aseme; (*FAINNA* SABAQATAKUM ILANNARI) – Na kwa hakika nishani yenu itakuwa moto. Zingatia hilo, undani wake wastaajabisha, na kina chake ni cha mbali, kizuri, na hivyo hivyo maneno yake mengi (a.s). Na katika baadhi ya nakala, imekuja ndani ya riwaya nyingine (WAS'SUBAQATUL AL JANATU) SIYNI ikiwa na 'dhummah,' na Subaqatu kwao ni jina la kitu ana– chopewa mshindi, kama vile mali au nishani mfano wa kikombe, na maana hizo mbili zipo karibu, kwa kuwa hiyo haiwi tuzo kwa kitendo cha jambo la kulaumiwa, bali huwa tuzo kwa ajili ya kitendo cha jambo linalohimidiwa.

---

1. Sijaona akalala mwenye kuitaka pepo, anasema: Ni miongoni mwa ajabu kubwa mno ambayo hajapata kuiona mfano wake ni ambaye anaamini kwamba kuna Jannah na utukufu wake, na kukamilika sababu za maisha ya furaha humo, vipi anaitaka na kisha analala! Na miongoni mwa maajabu makubwa, ni ambaye ana yakini na Moto, na kutisha kwake, na ni mkusanyiko wa sababu za mashaka, vipi haukimbii bali analala! Yaani, haimpasi alale mtakaji wa hii wala mkimbiaji wa hii.
2. Manufaa yote sahihi yapo katika haki tu, endapo msemaji atasema kuwa: haki haikum–nufaisha, hivyo batili ni yenye kumdhuru mno. Na ambaye haukumnyoosha mwongozo wa mwongozaji kuielekea haki, yaani, haikumfikisha kwenye utashi wake wa maisha mema, upotofu utamkokota kwenye limbi la maangamizi.
3. Msafara ni kuiacha dunia, na tumeamrishwa nao ni amri ya kimaumbile, yaani kama Mungu alivyotuumba, ametuumbia kuyaacha maisha ya dunia ili tukakae milele akhera, na masurufu aliyotuonyesha ni matendo mema na kuacha maovu.

29. Na Miongoni Mwa Khutba Zake (A.S)

Katika kuwalaumu wafanyao visingizio

"Enyi watu (mlio kama wale ambao) miili yao iko pamoja, wenye kutofautiana matakwa yao, maneno yenu yalainisha mawe magumu kabisa, na vitendo vyenu vyawatumainisha kwenu maadui! Kwenye vikao mwasema hili na lile, vita vikija mwasema tokomea mbali.

Wito wa mwenye kuwaiteni haupewi sikio wala moyo wa mwenye kuwachukulieni kwa nguvu hauwi na utulivu. Nyudhuru zisizo na maana. Mliniomba kurefusha muda, ni ulipaji wa mwenye deni msogeza muda, dhaifu hawezi kuizuia dhulma, na haki haipatikani ila kwa juhudi. Ni nyumba gani mtailinda baada ya nyumba yenu hii! Na kiongozi (imam) gani baada yangu mtaweza kupigana pamoja naye?

Wallahi aliyedanganyika ni yule mliyemdanganya, na mwenye kufaulu nanyi atakuwa amefaulu – Wallahi – na mshale usiofanikisha.1 Na mwenye kutupa na ninyi atakuwa ametupa kwa mshale uliovunjika maingiliyo ya kamba, Wallahi nimekuwa sisadiki kauli yenu, na wala situ– mainii nusra yenu, wala simkamii adui kwa kuwatumainia ninyi. Mmekuwaje? Dawa yenu nini? Nini tiba yenu? Hao watu ni wanamume kama ninyi. Ni kauli tupu bila ya ilmu, na mghafiliko bila ya kujiepusha, na tamaa katika ambalo si haki!?"

1. Mwenye kufanikiwa na ninyi na mkawa hisa yake, atakuwa amefanikiwa na mshale usiofaa, nao ni mshale wa ramli usiokuwa na hadhi.

30. Na Miongoni Mwa Semi Zake (A.S)

Kuhusu maana ya kumuuwa Uthman:

“Lau ningeamuru hilo ningekuwa muuwaji, na lau ningekataza ningekuwa mwenye kunusuru,1 ila ni ukweli kuwa aliyemnusuru hawezi kusema kuwa: Ametelekezwa na ambaye mimi ni bora kuliko yeye, na aliyemtelekeza hawezi kusema: Amemnusuru ambaye ni bora kuliko mimi.2

Na mimi nayajumlisha mambo yake kwenu. Amejitwalia na kuyatumia vibaya aliyoyatwaa. Na mmekosa uvumilivu, mkafanya vibaya kutovumilia kwenu.3 Na Mungu anayo hukumu muwafaka kwa mwenye kujitwalia na mtovu wa uvumilivu”.

1. Anasema: Kwa hakika yeye hakutoa amri ya kuuliwa Uthman, lau angefanya hivyo angekuwa muuwaji, na hali halisi yeye hana hatia ya mauwaji yake. Na wala hakukataza, yaani hakumlinda kwa upanga wake wala hakupigana badala yake, vinginevyo angekuwa mwenye kumnusuru. Ama kukataza asiuliwe kwa ulimi wake, ni jambo lililothibiti, kwani yeye ndiye aliyewaamuru Hasan na Husain wawaziwie watu mbali na yeye.

2. Ila ni ukweli kuwa aliyemnusuru… maana yake ni kuwa waliomtelekeza walikuwa bora kuliko waliomnusuru; kwa sababu waliomnusuru wengi miongoni mwao walikuwa mafasiki, mfano wa Marwan bin Al-Hakam na walio mfano wake. Na walio mtelekeza ni Muhajirun na Ansar. Kwa hiyo waliomnusuru hawakuwa bora zaidi yawaliomtelekeza. Kwa ajili hiyo aliyemnusuru hawezi kusema mimi ni bora kuliko aliyemtelekeza, wala hawezi aliyemtelekeza kusema kuwa: Mwenye kumnusuru ni bora kuliko mimi, anakusudia nyoyo zimeafikiana kuwa waliomnusuru hawakuwa na ubora wowote juu ya waliomtelekeza.

3. (Waanaa jamiun lakum amrahu.....) mpaka mwisho wa mlango, maana yake ni kwamba yeye Uthman amefanya lisilofaa, na ninyi mmefanya lisilofaa, ama yeye amejitwalia akafanya vibaya, yaani aliyahodhi mambo akafanya vibaya katika kuhodhi, na ilikuwa inambidi afanye wepesi ili asikuudhini, ama ninyi mlikosa subira kwa aliyoyafanya, yaani mlihuzunika mkafanya vibaya katika huzuni; kwa sababu ninyi mmemuua, hamkufanya upole katika kukatishwa tamaa kwenu wala hamkusimama kwenye mpaka ulio bora kwenu, ilikuwa inawabidi muishie kulalamika, wala msiende kwenye kufanya ubaya kiasi cha kuua, na Mungu anayo hukumu kumhusu aliyehodhi, naye ni Uthman, na aliyekatishwa tamaa, nao ni ninyi, imma amchukulie yeye na awachukulie ninyi au amsamehe na awasamehe ninyi.

31. Na Miongoni Mwa Semi Zake (A.S)

Kwa ibni Abbas:

Alipomtuma kwa Zubairi akimtaka arejee kwenye utii wake kabla ya vita vya Jamal:

“Usikutane na Talha, kwa kuwa wewe endapo utakutana naye utamkuta yuko kama ng’ombe maksai amezipindisha pembe zake, anayaparamia magumu huku akisema: ‘Ni mepesi hayo,’ lakini kutana na Zubair, kwa kuwa yeye ana tabia laini, na umwambie: ‘Mtoto wa mjomba wako anasema: Ulinitambua toka Hijazi,1 na hunitambui Iraq, ni jambo gani limebadilisha yaliokudhihirikia!”

Maelezo: Amesema Ar-Radhiy (r.a.): Yeye (a.s) ni wa kwanza ambaye limesikika neno hili kutoka kwake, nakusudia: (*Famaa ada mimmaa badaa*) – nini kimemtoa mbali na lililomdhirihikia.

---

1. Arifahu bil-Hijazi: Alimtii huko kwa kuwa alimfanyia bai’ya, na akaacha kumtambua huko Iraqi kwa kuwa alitoka dhidi yake na alikusanya watu ili kumpiga vita.

32. Na Miongoni Mwa Khutba Zake (A.S)

Kuhusu dhulma ya zama:

“Enyi watu, kwa kweli sisi tupo katika muda wa dhulma na zama za kufuru,1 mwema humo ahesabika muovu, na dhalimu huzidi humo kiburi, hatunufaiki na tulilojua, wala hatuulizi tusilolijua wala hatuogopi msiba mpaka utufike, na watu wako aina nne: Miongoni mwao kuna ambaye hakuna kinachomzuia kufanya ufisadi katika ardhi isipokuwa unyonge wa nafsi yake na ubutu wa silaha zake na uchache wa mali yake.

Na miongoni mwao kuna mwenye kujitokeza na upanga wake na kuitangaza shari yake, na ambaye ameleta askari wake wapanda farasi na askari wake waendao kwa miguu, ameiandaa nafsi yake kwa shari na ufisadi, ameiangamiza dini yake kwa ajili ya mali yenye kuvunjika afaidikayo nayo haraka, au kundi la farasi analolichunga au mimbari aipandayo.2

Biashara mbaya ni kuiona dunia kuwa ina thamani kwa ajili yako, na uliy- onayo yatakuwa fidia kwa Mungu!

Na miongoni mwao kuna ambaye aitaka dunia kwa kazi ya akhera, wala haitafuti akhera kwa kazi ya

dunia, ameishusha chini haiba yake, na kuzifanya hatua zake karibu, na kupania nguo yake, na amejipamba nafsi yake ili aaminike, na ameifanya sitara ya Mungu kuwa ni kichaka cha kufanyia maasi.3

Na miongoni mwao kuna ambaye unyonge wa nafsi yake umemuweka mbali na kuutaka ufalme,4 na kukatika kwa sababu zake, hali hii imemzuia kuifikia nafasi yake, kutokana na hali hiyo akajipamba kwa jina la kutosheka, na kujipamba na vazi la walioipa nyongo dunia, na katika hilo hana safari ya matembezi ya jioni wala asubuhi.

Na wamebakia watu ambao kumbukumbu ya marejeo imeyafumba macho yao,5 na woga wa kukusanywa umebubujisha machozi yao, (kukusanywa baada ya kufufuliwa watu Siku ya Kiyama), kwa hiyo wao wapo kati ya mwenye kukimbia kiasi cha kujitenga, na mwenye kuogopa aliyekandamizwa, na aliye kimya aliyefumbwa mdomo, na mlinganiaji aliye na ikhlasi, na mwenye kuhuzunika na anayeumia.

Taqiiya imewazimisha,6 wamekumbwa na udhalili, hivyo wao wako ndani ya bahari ya chumvi,7 vinywa vyao vimenyamaza, na nyoyo zao zimejeruhiwa. Wamewaidhi mpaka wamechoka, wamekandamizwa mpaka wamekuwa dhalili, na wameuliwa mpaka wamebaki wachache.

Dunia iwe kitu kidogo machoni mwenu kuliko majani ya mti yaliyopukutika, na mabaki ya manyoya ya ngamia yaliyotindwa.8 Waidhikeni na waliokuwa kabla yenu, kabla hawajawaidhika na ninyi wale watakao kuwa baada yenu, ikataeni dunia ikiwa ni ya kulaumiwa, kwa kuwa hiyo imewakataa walioipenda zaidi kuliko ninyi.

Maelezo: Amesema Ar-Radhiy: Hutba hii huenda asiyejua akainasibisha na Muawiya; hali ikiwa ni miongoni mwa manemo ya Amirul-Mu'uminina (a.s) yasiyo na shaka. Basi wapi na wapi dhahabu na udongo! Na wapi na wapi maji baridi na ya chumvi! Na hilo limethibitishwa na dalili yenye umahiri. Na mkosoaji mwerevu Amr bin Bahri Al'Jahidh, amekosoa hilo kwa kuwa yeye ameitaja hutba hii ndani ya kitabu *Al-Bayan wat-Tabyiin* na amemtaja aliyeinasibisha na Muawiyah, kisha aliongea baada yake maneno kuhusu maana yake, kwa ujumla wake ni kuwa yeye alisema: "Maneno haya yashabihiyana mno na maneno ya Ali (a.s) na madhehebu yake katika kuzigawa aina za watu, na katika kutoa habari ya walivyo miongoni mwa makandamizo na udhalili, na miongoni mwa Taqiiyah na hofu yalingana mno." Amesema: "Basi lini tumemkuta Muawiyah katika hali miongoni mwa hali, na katika usemi wake akienda mwenendo wa watu wenye zuhdi mwenendo wa wachamungu!"

---

1. Al-Kanuudu: yaani kafiri mno. Na huelezwa (kwenye riwaya nyingine) Wa zamanun shadiidu, yaani, zama zenye ubakhili: Kama ilivyo katika kauli Yake Ta'ala: (Wa innahul hubil khair lashadiidu – kwa hakika yeye hupenda kheri mno – al-Aadiyat: 8). Yaani, kwa hakika mwanadamu, kwa sababu ya kupenda kwake mali, ni bakhili, na sifa ni ya watu wa zama na dahari kama ilivyo dhahiri. Na ubaya wa tabia za watu, huwafanya kumhesabu mtu mwema kuwa ni mbaya.
2. Mimbari aipandayo: Yaani, katika kupanda mimbari na kuwahutubia watu ni miongoni mwa daraja ya juu inayomfanya mtu aitafute, kwa hiyo sehemu hii ya vitu au ya watu ime- haribu watu katika kutafuta umashuhuri huu uliotajwa.
3. Kichaka: Na hili ni kundi la tatu.

4. Na hili ni kundi la nne, wala si katika kuipa nyongo dunia, si katika kutenda wala kuacha.
5. Hili ni kundi la tano la watu wote, na makundi manne ya watu walio maarufu walio katika maono ya watu wa kawaida, hivyo basi kauli yake ya hapo mwanzo (watu ni makundi manne) anakusudia kwayo ambao wanajulikana kwa mtazamo wa wazi wa watu, ama watu ambao waliofumba macho mbali na tamaa za dunia; kwa kuiogopa akhera, na kukum– buka kwao marejeo yao, hawa hawajulikani kwa watu wa kawaida, ila tu hutambuliwa hali zao na walio mfano wao, hivyo kana kwamba wao katika mtazamo wa watu, wao si watu.
6. Taqiiyah imewazimisha: Imeangusha utajo wao kiasi cha kuwa hawakumbukwi na watu. Na taqiiyah hapa ni kujikinga dhidi ya dhulma kwa kuificha hali halisi.
7. Wako katika bahari ya chumvi: Yaani wao kati ya watu ni kama aliyetumbukia katika bahari ya chunvi, hapati cha kuzima kiu yake wala.
8. Amewataka waidharau dunia baada ya mgao uliotangulia; kwa sababu imethibiti kuwa dunia haiko safi isipokuwa kwa watu wa shari, ama wachamungu aliowataja wao hawakuambua kitu kutoka dunia hii isipokuwa kutaabika, na kila ambaye hali yake ni kukimbilia kwa watu wa shari, na kujikausha mbele ya watu wa kheri basi yeye ndiye afaa mno kudharauliwa.

33. Na Miongoni Mwa Khutba Zake (A.S)

Alipokuwa akitoka ili kupigana na watu wa Basra:

Abdullah bin Abbas alisema: “Niliingia kwa Amirul’Mu’minina (a.s) alipokuwa Dhuqaar, 1naye akiwa yuashona ndara zake, akaniambia: “Nini thamani ya ndara hizi?” Nikamwambia: “Hazina thamani yoyote.” Akasema (a.s): “Wallahi hizi nazipenda mno kuliko uamiri wenu (ukhalifa) ila tu endapo nitatenda haki au kuzuia batili” Hatimae alitoka na kuwahutubia watu akisema:

Kwa kweli Mwenyezi Mungu swt. alimtuma Muhammad (s.a.w) hapakuwa na mmoja yeyote katika waarabu asoma Kitabu, wala kudai unabii, basi yeye akawaongoza watu mpaka aliwafanya wakae mahali mwao,2 na kuwafikisha kwenye uokovu wao, hivyo wakawa katika istiqama ndani ya Uislamu na kuimarika nyayo zao.3

Wallahi nilikuwa miongoni mwa waliokuwa wakiongoza, nikiwafurusha mpaka walitokomea wote, sikudhoofu wala sikuwa mwoga.

Kwa kweli mwendo wangu ni ule ule, Wallahi nitaitoboa batili mpaka haki ijitokeze pembezoni mwake.4 Wana nini makuraishi na mimi!

Wallahi niliwapiga vita wakiwa makafiri, na nitawapiga vita wakiwa wamedanganyika, kwa kweli mimi ni mwenzao wa hapo jana na ni mwenzao hii leo. Wallahi hawatuadhibu makuraishi ila ni kwa sababu Mungu ametuchagua juu yao, na tumewaingiza ndani ya mamlaka yetu, kwa hiyo wamekuwa kama alivyosema wa kwanza (mshairi):

“Kwa maisha yangu, ungali wanywa maziwa mapya asubuhi,

Na kula kwako tende kwa jibini.

“Sisi ndio tuliokupa daraja, wala hukuwa wa juu,
na kukuzungushia ulinzi (*kwa farasi*) *na mikuki.”*

---

1. Dhuqaar: Ni kitongoji kati ya Waasiti na mji wa Kufa, nacho kipo karibu na mji wa Basra, na hapo ilipiganwa vita kati ya waarabu na wafursi (wa-Irani), waarabu walipata nusra, hilo lilikuwa kabla ya Uislamu.
2. Kukaa mahali mwao, kwamaanisha watu kabla ya Uislamu kana kwamba walikuwa wageni waliosambaratishwa, na Uislamu ndiyo nyumba yao wanayoishi na kuwa na amani bila ya hofu, kwa hiyo Nabii (s.a.w.w.) amewaongoza watu mpaka amewafikisha nyumbani mwao – Uislamu – kwamba walikuwa wamepotea mbali nao, aliwafikisha mahali pao pa uokovu mbali na kuangamia.
3. Ukatuama mpini wao: Yaani walituama ndani ya Uislam, yaani mpini wao ulikuwa umepinda ukanyooka, na Qaana: mpini na mkuki, na maneno haya ni mfano wa kunyooka kwa hali zao.
4. Wallahi nitaitoboa batili: Kana kwamba ameifanya batili ni kitu kimeizingira haki na kuificha, na haki ikawa iko ndani mwake kama kitu kilichojificha na kujistiri humo, hivyo basi akaapa kuitoboa ile batili mpaka haki ijitokeze pembezoni mwake, batili inakimbilia kwenye dhana na kuishughulisha mbali na haki, na inakuwa kizuizi kinachozuia uoni wa haki, kwa hiyo ni kama kitu kimeienea haki na kuificha, na haki inakuwa katika mficho wake. Na maneno haya ni methali ya hali ya batili na haki, na hali ya Imam katika kuifichua batili na kuidhihirisha haki.

34. Na Miongoni Mwa Khutba Zake

Katika kuwaandaa watu ili kuwakabili watu wa Sham:

“Ole wenu! Kwa kweli nimechoka kuwakemea! Je mmeridhika na maisha ya dunia yawe badala ya akhera na unyonge mahali pa utukufu? Endapo nikiwaita kumpiga vita adui yenu, macho yenu huzunguka kana kwamba mmefunikwa na mauti na kutokwa na fahamu kwa (kufunikwa na mauti).

Hufungika kwenu hutba yangu, kwa hiyo mnakanganyikiwa kana kwamba nyoyo zenu zimepagawa kwa hiyo hamuitii akilini. Ninyi kwangu hamuaminiki kamwe. Ninyi si nguzo itegemewayo, ninyi sio jamaa wa kuhitajiwa. Ninyi mko mfano wa ngamia ambao wachungaji wake wamepotea, kila wakusanywapo upande mmoja wanatawanyika upande mwingine, Wallahi wachochezi wabaya wa vita ni ninyi! Mnachokozwa wala hampigani, ncha zenu zinapunguzwa wala hamghadhibiki; adui halali na akawaacha na hali ninyi mpo katika mghafala mmesahau. Wallahi wamezidiwa wenye kutelekezana.

Wallahi mimi nakudhanieni endapo vita vitakuwa vikali, na mauti ikawa imeshika kasi mtakuwa mmejitenga na ibn Abi Talib kama kinavyojitenga kichwa.

Wallahi kwa kweli mtu anatoa mwanya kwa adui yake; anakuwa yu aila nyama yake, na anavunja mfupa wake na anachana ngozi yake, (huyu) kushindwa kwake ni kukubwa mno, kilichokusanya pande za kifua

chake ni dhaifu (yaani yeye ni dhaifu). Wewe kuwa yeye ukipenda; ama mimi Wallahi simwezeshi binafsi adui yangu... viganja na nyayo zitadondoka na baada ya hivyo Mungu atafanya apendavyo.

Enyi watu, kwa hakika mimi nina haki juu yenu na ninyi mna haki juu yangu: Na haki yenu juu yangu ni kuwapeni nasaha, na kuwarahisishia ruzuku zenu, na kuwaelimisheni ili msiwe wajinga, na kuwaadabisheni ili mjue. Ama haki yangu juu yenu ni kuitekeleza bai'a, na nasaha mbele ya macho yangu na mbali nayo, na kuniitika niwaitapo, na kutii ninapowaamrisha".

35. Na Miongoni Mwa Khutba Zake (A.S)

Baada ya hukumu (*tah'kiim*):

"Shukrani ni za Mwenyezi Mungu japo zama zilete misiba mizito na tukio zito na kubwa.1
Na ninashuhudia kuwa hapana mungu isipokuwa Allah Mungu Mmoja peke Yake hana mshirika, hayuko mungu mwingine pamoja na Yeye, na kuwa Muhammad (s.a.w.w) ni mja Wake na mjumbe Wake.

Ama ba'ad, kwa kweli kumuasi mtoa nasaha mwenye huruma alie mjuzi mwenye uzoefu kunarithisha hasara, na matokeo ya majuto. Nami nilikuwa nimewaamrisheni amri yangu kuhusiana na hukumu hii,2 na nilikuwa mnyofu kwenu, kwa kuwapa rai yangu iliyohifadhiwa, lau ingetiiwa amri ya Qasiir!3

Mlinikatalia ukataaji wa wapinzani wakakamavu, na waasi wasio watiifu, mpaka mtoaji wa nasaha akaishakia nasaha yake4 na kijiwe (kigumu kama cha kiberiti) kilishindwa kutoa cheche zake,5 hivyo nikawa mimi na nyinyi ni kama alivyosema yule mshairi Hawaazin.6

Nilikuamrisheni amri yangu huko Mun'arajil–Liwa
Nasaha haikubainika isipokuwa baadae asubuhi ya kesho yake".

---

1. Makusudio ya tukio kubwa hapa ni tukio la mahakimu wawili.

2. Hukumu hii hapa mradi wake ni hukumu ya mahakimu wawili: Amr bin Al'Aas na Abi Musa Al'Ash'ariy, na hii ilikuwa baada ya vita kusita kati ya Amirul'Mu'minina (Ali bin Abi Talib) na Muawiyah bin Abii Sufian katika vita vya Sifiin mwaka wa 37 A.H. Kwani jeshi la Muawiyah lilipoona limelemewa katika mapambano, Muawiyah alifanya udan– ganyifu kwa kuiangika misahafu (Qur'ani) juu ya mikuki akiomba ifanywe hukumu kwa mujibu wa Kitabu cha Mungu. Na vita vilikwishaangamiza watu wengi wa pande zote mbili, kwa hiyo wasomaji wa Qur'ani (al–Qurau) wakadanganyika, na kundi la watu likawafuata kutoka jeshi la Ali (a.s) wakasema: "Tumeitwa kwa Kitabu cha Mungu na sisi tunastahiki zaidi kukiitika." Amirul'Mu'minina (a.s) akawaambia: "Kwa kweli hilo ni neno la haki linalokusudiwa batili, kwa kweli wao hawakuiinua ili waitekeleze hukumu yake, wao wanaijua wala hawafanyi kwa muujibu wake, hiyo ni hadaa, unyonge na hila, niazi– meni mikono yenu na fuvu zenu kwa saa moja, haki imefikia makatio yake, hakuna kilicho baki ila ukatwe mwisho wa waliodhulumu."
Wakaenda kinyume na wakatofautiana, vita vikaisha, na watu wakaongea kuhusu suluhu na tah'kiimu ya watu wawili wahukumu kwa yaliyo ndani ya Kitabu cha Mungu. Kwa hiyo Muawiyah alimteua Amr bin Al–Aas, na watu wa

Amirul'Mu'minina wakamchagua Abu Musa Al'Ash'ariy, Amirul'Mu'minina hakuridhika na uteuzi huu, na badala yake alimch– agua Abdullah bin Abbas, wao hawakuridhika. Kisha alimchaguwa Malik Al'Ash'tar an– Nakh'i lakini hawakutii, akaafikiana nao uchaguzi wa Abu Musa Al'Ash'ariy akiwa amekirihishwa, baada ya kuwa alitaka udhuru katika kuwanasihi hawakutii, akawaacha; yaani alifanya ikhlas rai yake kuhusiana na suala la hukumu kwanza na mwisho, kisha suala la hukumu liliishia Abu Musa kufanyiwa hadaa na Amri bin Al'Aas, hadaa ambayo ilim– fanya Abu Musa amuengue Amirul'Mu'minina. Hilo likasababisha kudhoofu kwa Amirul'Mu'minina na sahiba zake.

3. Yeye alikuwa mtwana wa Judhaima aliyekuwa maarufu kwa jina la Al'Abrash, alikuwa mwerevu. Alitoa ushauri kwa Bwana wake Judhaima kuwa asimwamini Zibaau Malikia wa Al–Jazira, akafanya kinyume na nasaha zake, na akamwendea ikiwa ni jibu la kutaka amuoe, yule malikia akamuua. Hapo ndipo Qasiir akasema: "Amri ya Qasiir haiti– iwi" tokea hapo ukawa mfano upigwao.

4. Mpaka mtoa nasaha akaishakia nasaha yake (mtoa nasaha hapa yu ajikusudia yeye mwenyewe), kwa kuwa wao walikula njama kwenda kinyume na nasaha yake mpaka akaingiwa na shaka na nasaha yake na akadhania labda nasaha haifai, na labda sahihi ni lile walilokubaliana! Na hiyo ni sera ya mwanadamu endapo upinzani utakithiri dhidi ya yaliyo sahihi, mkweli hujituhumu binafsi.

5. Kijiwe kilishindwa kutoa cheche zake: Yaani yeye baada ya hivyo haoni kuwa na rai iliyo sahihi kutokana na kukithiri kwa upinzani wao aliokutana nao, hali huwa hivyo kwa kila mtoa shauri mnasihi, akituhumiwa uoni wake hufifia na rai yake huharibika.

6. Akhu Hawaazin: Yeye ni Duraid bin As–Simmah. Na Muna'ariju'liwa: Ni jina la mahali, na asili ya Liwa: ni mchanga mpya baada ya mchanga.

36. Na Miongoni Mwa Khutba Zake (A.S)

Katika kuwahofisha watu wa An–Nah'rawan:[1]

Mimi ni mwonyaji kwenu, nakutahadharisheni msije kuwa waliotupwa chini wafu katika mto huu, na ardhi tulivu ya chini bila ya ubainifu wowote kutoka kwa Mola wenu Mlezi, wala hoja ya nguvu mliyonayo, mmekuwa katika myumbo na kudra imewatieni kamba.

Na nilikuwa nimewakatazeni hukumu hii – maamuzi mliyoyafanya – mkanikatalia ukataaji wa wapinzani wanaotupilia mbali, kiasi cha kunifanya niichukue rai yangu na kuitia kwenye utashi (potovu) wa nafsi zenu, na hali ninyi mkiwa wapumbavu wa akili – hamna baba – Mungu awaangamize! katika kuwakatazeni hukumu ile, sijawatakieni madhara yeyote.

---

1. An–Nah'rawani: Ni jina la sehemu chini ya mto kati ya Al'Khafiqu na Tarafa'u, ulio karibu na mji wa Kufa upande wa jangwa la Haruurau. Na huitwa eneo la juu ya mto huo Taamir. Na ambao walikuwa wametoka dhidi ya utii wa Amirul'Mu'minina na wakamkosoa kuhusu tah'kiim na wakatangua Ba'ia yake, na walidhihirisha uadui wao kwake, na wakawa na vita dhidi yake, kwa hiyo wengi wao walijikusanya mahali hapo. Na wao wanaitwa ma–Haruriyah; kwa maelezo yaliyotangulia sababu ardhi ambayo walijiku– sanya ilikuwa inaitwa Haruura'u, na kiongozi wa kikundi hiki kipotovu Hur'qus bin Zahiir Assa'adiy, na laqabu yake ni Athudayyatu, dogesho la neno thadyu, Amirul'Mu'minina ali– watokea akiwawaidhi kuwataka wabatilishe usemi wao, na kuirejea Bai'a yao, kwa hiyo waliijibu nasaha hii kwa kuvurumisha mishale, na kuwauwa sahaba wake karrama Ilahu waj'hahu,Hapo ndipo aliamrisha wapigwe vita, kwa hiyo mapigano yalitanguliwa na

onyo hili tunaloliona.

37. Na Miongoni Mwa Semi Zake (A.S)

Usemi huu waenda mwendo wa khutba:1

Na humo (a.s) anataja fadhaili zake aliisema baada ya tukio la An-Nah'rawan:

Nilitekeleza amri walipokuwa wameshindwa2…na nilijitokeza walipofichama, na nilitamka waliponyamaza, nilipita kwa nuru ya Mungu waliposimama. Nilikuwa wa sauti ya chini mno kati yao, na wajuu mno kwa kwenda mbele, na niliruka na hatamu zake, na nilikuwa wapekee kuikabili khatari iliyokuwa ikiepukwa. Na nilikuwa kama jabali halitikiswi na upepo mkali wala haimuondoi dhoruba. Yeyote hakuwa na la kuniaibisha nalo, wala msemaji hakuwa na la kunikebehi (yaani sikuwa na aibu mtu awezayo kuniaibisha nayo).3

Mnyonge kwangu ni mwenye hadhi mpaka nimrudishie haki yake, na mwenye nguvu kwangu ni dhaifu nitaichukuwa haki aliyodhulumu kutoka kwake.

Tumeyaridhia maamuzi yake Mungu,4 na tumesalimu amri yake Mungu. Je, mwaona mimi nimsemee uwongo Mjumbe wa Mungu (s.a.w.w)? Wallahi mimi ndimi wa kwanza kumsadiki, sitokuwa wa kwanza kumsemea uwongo. Niliangalia suala langu, na kuona utii wangu yapasa uitangulie ba'iah yangu, hali ikiwa ahadi yangu imekuwa mzigo shingoni mwangu.5

---

1. Usemi huu Ar-Radhiy ameuleta kana kwamba ni kipande kimoja chenye lengo moja, wala sivyo, ni kipande hakikurubiani. Kila kipande miongoni mwavyo kina maana isiyokuwa kwenye kipande kingine. Ar-Radhiy (r.a) alikidondoa kutoka kwenye maneno ya Amirul'Muuminina (a.s) marefu yaliotawanyika, aliasema baada ya tukio la An- Nah'rawan, humo aliieleza hali yake tokea alipotawafu Mtume wa Mungu (s.a.w.w.) mpaka mwisho wa wakati. Kwa hiyo Ar-Radhiy akavifanya alivyovidondoa miongoni mwavyo kimoja kimoja, na vimekuwa kwa msikilizaji kana kwamba kwavyo yu-alenga lengo moja. Nayo imo katika milango minne; wa kwanza: Kauli yake: " fa qumtu bil'am- ri" mpaka kauli yake: "wastadarta burhanaha." Na mlango wa pili tokea kauli yake: "Kal-jabali la tuhariquhu al-qawaswifu," mpaka kauli yake: "hatta akhadhal-haqa minhu." Na mlango wa tatu: tokea kauli yake: "radhwiina anillahi qadhwa'ahu." Mpaka qauli yake: "fala akunu awwala man kadhaba alayhi." Na mlango wa nne: yaliobakia.

2. Yaani nilikataza munkari waliposhindwa sahaba wa Muhammad (s.a.w.w) kufanya hivyo. Anaielezea hali yake kipindi cha ukhalifa wa Uthman, na nafasi yake katika kuam- risha mema na kukataza munkari (mabaya) siku za matukio, yaani yeye alikataza munkari waliposhindwa kaumu.

3. Na huu ni mlango wa pili anataja hali yake baada ya Ba'iah kuwa yeye aliutekeleza ukhalifa akiwa kama jabali….

4. Kauli yake: (Radhwiinaa…) ni maneno aliyasema alipokuwa akikagua kaumu kwa makini katika askari wake kuwa wao wanamtuhumu katika anayowapa habari kutoka kwa Nabii kuhusu habari za mapambano na mambo ya ghaibu.

5. Usemi wake"Niliangalia kuhusu suala langu": Jumla hii ni kipande kutoka usemi wake kuhusu hali yake binafsi (ilivyokuwa) baada ya kutawafu Mtume wa Mungu (s.a.w.w.), alibainisha kuwa aliamriwa awe mpole katika kuitaka haki

yake, akaitii amri katika ba'ia ya Abu Bakar, Umar na Uthman kwa kulinyamazia hilo.

38. Na Miongoni Mwa Khutba Zake (A.S)

Akielezea maana ya shub'hah (kushabihiana):

Shub'ha imeitwa hivyo kwa sababu inashabihiana na ukweli, ama wapenzi wa Mungu, mwanga wao humo ni yakini, na dalili yao humo ni nji ya mwongozo. Ama maadui wa Mungu wito wao humo ni upotovu, na dalili yao ni upofu. Hatoepuka umauti mwenye kuuogopa.1

---

1. Usemi wake: "hatoepuka umauti..." hauna uwiano na usemi wa kabla yake, usemi huo ni kipande cha maneno mengine amekiambatanisha na huu kama alivyokusanya milango iliyotangulia.

39. Na Miongoni Mwa Khutba Zake (A.S)

Kuwalaumu wanaobaki bila ya kwenda vitani:

Nimekumbwa na balaa la wasiotii nitoapo amri, wala hawaitikii nikiita. Hamna baba! Mnangoja nini kwa kumnusuru Mola wenu?

Hapana dini iwezayo kuwakusanya, wala hisia ya aibu kuwaghadhibisheni! Nasimama kati yenu nikiomba nusra, na nakuiteni nikiomba usaidizi, wala hamnisikilizi usemi wowote, wala kunitii amri, mpaka yafichuke matokeo mabaya! Kisasi hakilipwi pamoja na ninyi, wala lengo halifikiwi pamoja na ninyi. Niliwaita ili muwanusuru ndugu zenu mkakoroma mkoromo wa ngamia aliyepatwa na maradhi ... na mkawa wazito kama uzito wa ngamia aliyekonda mwenye kujeruhiwa kisha nikajiwa na kikosi kutoka kwenu, dhaifu kikinepanepa; (**Kana kwamba wanasukumwa kwenye mauti nao wanaona; 8:6**)

Maelezo: Ar-Radhiy (r.a) amesema: Usemi wake (a.s): (*mutadhai-bun*) yaani yenye kuyumbayumba; kutokana na kauli yao: (*tad- ha'abati riihu*) yaani upepo umeyumbayumba, uvumapo ukiyumba, kutokana nalo hilo mbwa mwitu amepewa jina hilo kwa sababu ya kuyumbayumba mwendo wake.

40. Na Miongoni Mwa Maneno Yake (A.S)

Kuhusu Khawariji alipoisikia kauli yao: "Hakuna hukumu ila ya Allah"

Na neno ni la kweli lakini linakusudiwa batili! Naam ni kweli kuwa hapana hukumu ila ni ya Mungu, lakini hao wanasema: Hapana uamiri ila wa Mungu. Na kwa kweli watu hapana budi wawe na mtawala mwema au muovu,1 mu'umin atenda (mema) katika utawala wake,2 na kafiri anastarehe humo, na Mungu aufikisha humo muda,3 na hukusanywa (kwa utawala wake) kodi, pamoja na yeye hupigwa vita adui, pamoja naye njia zabakia na amani, pamoja naye huchukuliwa (haki zilizodhulumiwa) kutoka kwa mwenye nguvu kwa ajili ya mnyonge; Ili mwema apumzike na ili muovu apumzishwe

Na katika riwaya nyigine ni kuwa yeye (a.s) aliposikia hukumu yao akasema:

"Hukumu ya Mungu naingoja iwe kwenu."

Na akasema: "Ama utawala mwema mchamungu humo hutenda mema, ama utawala muovu hustarehe humo mwenye mashaka (*shaqiy*); mpaka muda wake ukatike na mauti yake imkute".

---

1. Ni dalili ya kuwa dhana yao batili kuwa hapana utawala ila ni wa Mungu ni: Hali ya dhahiri yaamua kuwa watu hapana budi wawe na mtawala mwema au muovu; ili mambo yao yanyooke. Na utawala wa muovu haumzuii mu'umini kutenda matendo yake (ya kiimani) ili kuilinda dini yake na dunia yake, na humo kafiri anastarehe mpaka ajali imchukue, na Mungu ayafikishe mambo muda wake uliopangiwa kulingana na nidhamu ya kimaumbile. Na maslahi zilizotajwa ziendelee. Na yawezekana ikawa kusudio la mu'umi– ni hapa ni amiri mwema na mradi wa kafiri ni mtawala muovu, kama ijulishavyo riwaya nyingine. Na kauli yake
2. Mu'min anafanya humo, yaani si kizuizi kwa mu'min kufanya: kwa sababu anaweza kuswali, akafunga, na kutoa sadaka japo kuwa mtawala ni muovu. Na kafiri akastarehe humo: yaani akastarehe na muda wake.
3. Na Mungu anaufikisha muda humo; kwa sababu utawala wa muovu ni kama utawala wa mwema, kwamba muda uliowekwa mwanadamu utaisha humo.

41. Na Miongoni Mwa Khutba Zake (A.S)

Na miongoni mwa Khutba yake (a.s) – Ameitaja ibn Talha katika kitabu Matalibus–Su'ul, Jz. 1, uk. 170

Kuhusu utekelezaji na ukweli:

"Enyi watu! Kwa kweli kutekeleza ahadi ni pacha wa ukweli,1 siijui kinga yenye kuhifadhi mno kuliko hiyo (kwa shambulio la dhambi) wala hafanyi uhaini mwenye kujua marejeo yalivyo.2

Kwa kweli tumeingia katika wakati ambao walio wengi miongoni mwa watu wake wameufanya uhaini kuwa ni uwerevu, na wajinga wamewanasibisha watu kama hao kuwa huo ni ujanja mzuri. Wamekuwaje (watu hawa)! Mungu awaangamize!

Na mwenye uzoefu na uelewa wa mambo ya maisha anao udhuru wa kumzuia asitekeleze amri na makatazo yake Mungu, lakini hautilii maanani ingawaje anao uwezo, akawa yu ajua hila, na pembeni mwake kuna kizuizi miongoni mwa amri ya Mungu na katazo lake lakini anaacha baada ya kuwa alikuwa na uwezo wa kutenda hayo, na huitumia fursa hiyo asiye na kizuizi cha kidini.

---

1. Kutekeleza ahadi ni pacha wa ukweli: Kwa kuwa utekelezaji ahadi hakika yake ni ukweli; na sidqu ambao ndio ukweli, kwani ukweli na utekelezaji ahadi kuwa kwao ni nira, mmoja hamtangulii mwenzake katika kuwa wala daraja.
2. Yaani mwenye kuijua akhera na ajua kuwa marejeo yake ni kwa Mungu naye ni Mwepesi wa kuhasibu hawezi kuhaini; kwa sababu uhaini unaharibu imani.

42. Na Katika Jumla Ya Usemi Wake (A.S)

Katika kuyafuata matamanio na kuwa na matumaini marefu:

Enyi watu! Kwa kweli niliogopalo zaidi juu yenu ni vitu viwili:

1. Kuyafuata matamanio

2. Na kuwa na matumaini ya muda mrefu1

Ama kuyafuata matamanio kunazuia haki, na kuwa na matumaini ya muda mrefu kunasahaulisha akhera. Oh, jueni kuwa dunia imepita haraka sana; hakuna kilichobaki humo ila mabaki mfano wa mabaki ya maji katika chombo ambacho maji yake yamemwagwa na mmwagaji wake.

Oh! jueni kuwa akhera imewadia, na kila mmoja wao anao watoto, basi ni bora muwe miongoni mwa wana wa akhera, na wala msiwe miongoni mwa wana wa dunia; kwa kuwa kila mwana atakutanishwa na mama yake Siku ya Kiyama, kwa kweli leo ni siku ya matendo na wala hapana hesabu na kesho ni hesabu tu hakutokuwa na matendo".

---

1. Tuulul'amalu, kuwa na matumaini ya muda mrefu ni kujidhania kuwa muda wa maisha ni mrefu kwa hiyo nitasali nitafunga nita nita.....kwa kujimwaga na raha ya dunia ambayo ni ya muda mfupi, huku mtu yu ajiliwaza nafsi yake kuwa anayoyaacha atayadiri– ki na kuyatekeleza yote bila ya wasiwasi hapo baadae, na hii ni sifa mbaya mno. Ama nguvu ya matumaini ya kufanikisha mema, kwa kuwa na yakini na msaada wa Mwenyeezi Mungu, huo ni uhai wa kila jema na ni

lenye kuleta matukufu. Na walionyimwa hilo wamekatishwa tamaa na rehema ya Mungu, waweza kuwadhania wako hai hali wakiwa wafu hawana hisia.

43. Na Miongoni Mwa Maneno Yake (A.S)

Walimshauri Sahaba zake kujiandaa kwa vita baada ya kuwa alikwisha mtuma Jarir bin Abdillah Al'Bajaliyi kwa Muawiyah:

"Kwa kweli kujiandaa kwangu kuwapiga vita watu wa Sham hali Jarir akiwa kwao ni kuifunga Sham, na kuwatowa watu wake mbali na kheri endapo wataitaka.1

Lakini nimemuwekea Jarir wakati ambao hatobaki baada ya wakati huo, ila endapo atakuwa amehadaiwa au ameasi. Rai sahihi iko pamwe na utulivu, basi kuweni watulivu, wala sichukii kujiandaa kwenu.2

Kwa kweli nimelichunguza suala hili kwa undani kupitia pande zote sikuona njia nyingine ila ni vita au kuyakufuru aliyoyaleta Muhammad (s.a.w.w.). Kwa hakika umma huu ulikuwa na mtawala aliyezusha uzushi – alizua *bid'a* – aliwafanya watu wamkasirikie, na walisema, kisha walichemka na kubadilisha kila kitu.

---

1. Anasema (a.s.): Kuwa yeye alimtuma Jarir ampe habari Mu'awiyah na watu wa Sham kuwa wamfanyie ba'iya yeye Imam, na waingie katika utii wake, na hajakatishwa tamaa nao. Hivyo basi kujiandaa kwake kuwapiga vita, na kukusanya jeshi, na kulipeleka kwenye ardhi yao, ni kuifunga milango ya amani kwa watu wa Sham, na kuwaondolea kheri endapo wataitaka, hivyo basi rai sahihi ni kufanya upole. Lakini yeye hachukii kujiandaa, yaani kila mmoja ajiandae binafsi na yale anayoyahitajia katika vita kama vile silaha na mfano wake, na aiweke nafsi yake mbali na yanayomshughulisha mbali na vita lau ikitokea, kiasi kwamba akiitwa, asiwe goigoi kuitika, na asiwe na kinachomzuia kuikabili.
2. Kuwakatalia kwake kujiandaa na usemi wake: "Wala sichukii kujiandaa kwenu" si maneno yanayopingana; kwa kuwa alichukia kujionyesha kwao maandalizi na kusema wazi wazi, wala hakuchukia kujiandaa kwa siri. Na yawezekana isemwe kuwa alikuwa anachukia kujiandaa kwake mwenyewe binafsi, wala alikuwa hachukii kujiandaa kwa sahaba zake; na haya mawili yako mbalimbali. Na mtazamo huo ameuchagua Al–Qut'bu Ar–Rawandiy.

44. Na Miongoni Mwa Semi Zake (A.S)

Tabariy ameyataja ndani ya tarehe yake, Jz.6, uk. 65, na Ath– Thaqafiy ndani ya Al–Gharatu, na Al–Baladhuriy ndani ya Ansabul'ash'rafi, uk. 411. Masqalat bin Hubairat Ash–Shaibaniy alipokimbilia kwa Muawiyah, na alikuwa amekwishawanunua mateka wa Bani Naajiyata kutoka

kwa mfanyikazi wa Amirul'Mu'minina (a.s) na kuwaacha huru, na alipomdai mali ya malipo alimfanyia udanganyifu na akakimbilia Sham.[1]

"Mungu amuweke mbali na rehema Masqalah! Amefanya kitendo cha mabwana, na amekimbia ukimbiaji wa kitwana, kwa hiyo msifiaji wake hakutamka kwani amemnyamazisha, na wala mfanya wasifu wake hajaeleza kitu bali amemkemea, lau angebaki tungechukua kutoka kwake kile ambacho ni chepesi kwake kukilipa, na tungengoja kuzidi mali yake."

---

1. Al-Khuraitu bin Rashid An-Najiy alikuwa mmoja katika Bani Naajiyata na alikuwa pamoja na Amirul'Mu'minina katika vita vya Siffin, baada ya vita ya Siffin aliitangua ahadi yake, na alimlaumu katika suala la tah'kiim, na alitoka huku akiwaharibu watu na kuwashawishi waende kinyume (na Amirul'Mu'minina), Amirul'Mu'minina akamtumia kikosi akiwemo Ma'aqilu bin Qays Ar-Rayahiy ili kumpiga vita yeye na waliojiunga pamwe na yeye, kikosi kilimdiriki akiwa Saiful'bah'ri huko Uajemi, na baada ya kuitwa atubie na kukataa kukubali aliandamwa na kuuliwa, na waliuliwa pamwe na yeye wengi katika watu wa kaumu yake, na walichukuliwa mateka waliokutwa ndani ya msafara wao waume kwa wake na watoto, na walikuwa mateka mia tano. Na Ma'aqilu aliporudi na mateka, alimpitia Masqalah bin Hubayrah As-Shiibaniy, na alikuwa mtendaji mtumishi wa Ali katika Ardashiiri khurh. Wanawake na watoto walimlilia, na wanaume walipiga mayowe wakimsihi waachiwe, kwa hiyo akawanunua kutoka kwa Ma'aqil kwa dirham mia tano elfu, kisha alikataa kulipa kile kiwango, na madai ya malipo ya ile haki yalipo mtopea alikimbilia kwa Muawiyah chini ya sitara ya usiku.

45. Na Miongoni Mwa Khutba Zake (A.S)

Nayo ni miongoni mwa khutba ndefu alihutubia siku ya Eid al'Fitri, akiilaumu humo dunia:

"Sifa njema ni za Mwenyezi Mungu ambaye rehema Yake haikatishi tamaa, wala hakuna anayeepukana na neema Yake, wala haukatishi tamaa msamaha wake, wala hafanyiwi kiburi kwenye ibada yake, ambaye kwake haikosekani rehema, wala haachi kuwa na neema.

Dunia ni nyumba iliyokadiriwa kuisha, na watu wake kutoweka humo, nayo ni tamu, ya (rangi) kijani.[1] Na kwa kweli imemharakia mwenye kuitaka, na imejiangika moyoni mwa mwenye kuitamani. Ondokeni humo mkiwa na masurufu yaliyo bora,[2] wala msiombe humo zaidi ya linalotosha,[3] Wala msiombe kutoka humo zaidi ya mlo.

---

1. Ni tamu na rangi kijani: Maneno ya mfano, yaani kuifananisha dunia na kinachozoeleka na yapendwayo na nyoyo na kuburudika macho. Imechukuliwa kutoka kauli yake (s.a.w.w.): Kwa hakika dunia ni tamu rangi ya kijani, na kwa hakika Mungu amekuwekeni humo angalieni jinsi mtakavyotenda.
2. Yaani muwe na maandalizi yaliyo bora kwa mazuri mliyonayo, nayo ni tabia njema na matendo mema.
3. Yaani msiombe zaidi ya riziki inayokutosheni.

46. Na Katika Maneno Yake (A.S)

Alipoazimia safari ya Sham:

Oh, Ewe Allah! kwa hakika mimi ninajilinda kwako na mashaka ya safari, na huzuni ya marejeo, na ubaya wa mandhari katika watu wa ndani na mali na mtoto.

Oh Ewe Allah! Wewe ni mwenzi safarini, na wewe ndio wa kuachwa nyuma na familia, wala havikusanyi viwili hivi asiyekuwa wewe, 1 kwa kuwa mwenye kuachwa nyuma hawezi kuwa mwenzi safarini, na ambaye ni mwenzi safarini hawi muachwa nyuma.2

Sayyid ar-Radhiy (r.a.): "Na mwanzo wa maneno haya imeelezwa kutoka kwa Mjumbe wa Mungu (s.a.w.w.) na Amirul-Mu'mini (a.s.) ameyafuatilia kwa balagha zaidi, na kuyahitimishia kihitimisho kizuri, kwa usemi wake (*walaa yaj'mau'huma ghairuka*) mpaka mwisho wa mlango."

---

1. Maneno ya kwanza yameelezwa kutoka kwa Mtume wa Mungu (s.a.w.w.) ndani ya vitabu sahihi na ameyakamilisha Amirul'Mu'minna (a.s) kwa kauli yake: (wala havikusanyi viwili hivi mwingine asiyekuwa Wewe) kwa kuwa dhati ya Mungu (swt) huwa sawa kwake kati ya mahali na zama – yaani huwezi kusema hapa Mungu hayupo au wakati huu Mungu hayupo – hivyo basi nyumbani na safarini kuihusu dhati Yake (swt) ni sawa.
2. Dua hii ameitaja Nasr bin Muzahim katika Kitabu "Siffiin," na wengine miongoni mwa waelezaji wa Sira pia wameitaja. Aliomba dua hii Amirul-Mu'mini na (a.s) baada ya kuweka mguu wake juu ya kipando chake katika msafara kutoka nyumbani kwake mjini Kufa akielekea Sham (Syria) kwa ajili ya kupigana vita na Muawiyah na swahaba zake, na tukio hilo lilikuwa baada ya vita vya Jamal (Ngamia), kwa kuwa Muawiyah bin Abi Sufyan alimkinza Imam Ali (a.s) wala hakuingia katika bai'a yake, na alibuni madai ya damu ya Uthman, hivyo watu wa Sham walivutwa na madai hayo, aliwaomba nusra kwa ajili ya rai yake, wakampa nguvu ya kwenda kinyume. Hivyo basi Amirul-Mu'uminina akafanya safari kumwendea, na walikutana mahali pakiitwa Siffiin. Walipambana muda si mfupi, vitaviliishia katika tah'kiimu ya mahakimu wawili: Amru bin Al'Aas na Abii Musa Al-Ash'ariy.

47. Na Miongoni Mwa Maneno Yake (A.S)

Katika kuuelezea mji wa al-Kufa

"Ewe al-Kufa! nakuona kana kwamba unawambwa mfano wa ngozi iliyotiwa rangi (iliyodibaghiwa) katika soko la Ukaadhu1 unapambana na shida, na wakumbana na misukosuko, nami najua fika kuwa mjeuri anapo kukusudia kwa uovu Mungu humshughulisha na balaa au humtupia muuwaji."

1. Ukaadhu: Ni jina la soko la Waarabu hapo kale upande wa Makah lilikuwa jangwani katika eneo kati ya Nakh'latu na Ta'aifu, walikuwa wakijikusanya hapo kila mwaka mwanzoni mwa mwezi wa Dhulqaadah – mwezi wa kumi na moja – ili kujifaharisha – kila mmoja na alichonacho miongoni mwa ubora na uhodari wa ushairi, hivyo: ta'aqadhu ni kujifaharisha, soko lilichukua jina la yaliyokuwa yakifanyika hapo. Walikuwa wanabaki hapo mwezi huku wakifanya biashara na kufanya nishadi tenzi za mashairi. Abu Dhuaybi amesema:
(Kuba zikijengwa hapo Ukadhu, biashara huanza na maelfu hujikusanya. Ulipokuja Uislamu ulibomoa hayo, na mara nyingi ilikuwa yauzwa ngozi iliyodibaghiwa. likanasibishwa jina hilo. wal adiimu: ni ngozi iliyodibaghiwa, na jam'ul adiimi ni udumu, na huenda ikafanywa alaa adimati kama wasemevyo: Raghiifu wa arghifa, (watumaddina maddal–adimi) ni istiara kwa sababu ya kukabiliwa na maafa ya hapa na hapa.

48. Na Miongoni Mwa Khutba Zake (A.S)

Alipokuwa akienda Sham:

"Shukrani ni zake Mungu kila usiku uingiapo na giza linapokithiri, na shukrani ni za Mungu kila nyota inapojitokeza na kila inapozama. (Mungu amesema: Na shari ya giza la usiku liingiapo; 113:3). Na himidi ni ya Mungu hakosi kuneemesha, wala halipwi fadhila.

Kwa kweli nimekwisha tuma kikosi cha mbele cha jeshi, na nimewaamuru wabakie kwenye ukingo wa mto wa *Dajlah* (Tigris), mpaka wajiwe na amri yangu, nimeonelea niyavuke maji haya mpaka makazi madogo ya watu miongoni mwenu wanaokaa ukingo wa mto wa *Dajlah* (Tigris), ili niwasimamishe pamwe na ninyi mumwelekee adui yenu, na niwafanye wawe nyongeza ya nguvu kwenu."

Sharifu Ar–Radhiy anasema: 'Anakusudia (a.s) kwa neno *Miltaat* hapa, upande aliowaamuru wabakie; nao ni ukingo wa mto wa Furaat, nalo latumika pia kwa ukingo wa bahari. Na asili ya neno ni ardhi iliyo tambarare. Na yu akusudia kwa neno *nut'fah*: maji ya Furaati, na hiyo ni miongoni mwa ibara ya aina yake na ya ajabu.'

49. Na Miongoni Mwa Maneno Yake (A.S)

Kuhusu sifa ya Rububiya umola ulezi na ilimu ya Kiungu:

Mwenye kustahiki sifa ni Allah (swt) ambaye ameficha mambo yaliyofichikana, na yamejulishwa na dalili zilizo dhahiri, na amezuilika na jicho lenye kuona;1 hivyo basi hapana jicho la asiyemuona linalomkanusha2 wala moyo wa aliyemthibitisha unaomuona.3 Ametangulia katika kuwa juu hapana kitu kipo juu zaidi yake, na amesogea kwa ukaribu hapana kitu kilicho karibu mno kuliko Yeye.4 Hivyo basi si

kuwa juu mno kwake kumemuweka mbali na kitu katika viumbe Vyake, wala si ukaribu wake umewafanya viumbe wawe sawa naye katika mahali.5

Hajazijulisha akili mipaka ya sifa Zake, wala hakuzizuia kiasi cha kuwa mbali na wajibu wa kumtambua kwake, hivyo basi Yeye ndiye ambaye alama za kuwepo zamshuhudia, kwa kukiri moyo wa mwenye kupinga,6 Mungu yu aepuekana na wayasemayo wamshabihishao na wanaompinga, yu juu juu juu kabisa!"

---

1. Amezuilika na jicho lenye kuona (Anasema: Kuwa Yeye (swt) haonekani kwa uoni wa jicho, pamoja na hali hiyo haiwezekani kwa asiyemuona kwa jicho lake amkanushe (kuwa hayupo); kwa sababu kila kitu ni dalili ya kuwako kwake, si hivyo tu bali Yeye mwenyewe (swt) kuweko kwake ni dalili tosha.
2. Hapana jicho la asiyemuona linalomkanusha (yaani asiyemuona hamkanushi kwa kutegemea kutomuona kwake; kwa sababu ya kudhihiri dalili nyingi kumuhusu.
3. Wala hapana moyo wa aliyemthibitisha (kuwepo kwake) unaomuona (Yaani: hapana njia kwa aliethibitisha kuwepo Kwake ilimu yake imtambuwe kwa kuzizunguka hali Zake zote na maalumati Yake na matengenezo Yake, au amekusudia kuwa hakika ya dhati Yake haijulikani; kama walivyosema jamaa wahakiki. Yaani hapana njia kwa aliyemthibitisha kuwepo Kwake, ilimu yake imzunguke na kumjuwa hali Zake zote na maalumati Yake na matengenezo Yake, au amekusudia kuwa yeye haujulikani ukweli wa dhati yake; kama walivyosema kaumu ya watu miongoni mwa wahakiki. Na maneno haya yameelezwa kwa njia nyingine, wamesema kuihusu hutuba hii: (Hapana moyo wa asiyemuona unaomkanusha, wala jicho la aliyemthibitisha linalomuona), Nayo ndiyo muwafaka zaidi.
4. Amekuwa juu kuliko kila kitu kwa dhati Yake na ukamilifu Wake na utukufu Wake, na amekuwa karibu na kila kitu kwa ilimu Yake na irada Yake na kuvizunguka kwake na kuvi- tilia manani kwake, kwa hiyo hapana kitu isipokuwa Yeye yu pamoja nacho na hapana kitu kimbali naye.
5. Kuwa juu Kwake hakujamuweka mbali (Kuwa juu kwake hakulazimiani na mahali kwa kuwa mbali na vitu vyenye miili, wala ukaribu wake haulazimu kuwa sawa navyo kwa kuhitajia mahali na upande, kwa sababu kuwa juu Kwake na kukaribia Kwake sio katika sura ya sehemu na mahali.
6. Kwa kweli moyo wa mpingaji japo akanushe, ukanushaji wake sio kingine ila ni athari ya sababu za nje ya maumbile yake, na kudhihiri alama za kuwepo katika kumjulisha, moyo wa mpinzani hauwi na nguvu kuizuia taathira, kwa hiyo yeye haepuki kukiri kwa ukweli hasa, japo kujitokeze kukanusha katika maneno yake na baadhi ya matendo yake.

50. Miongoni Mwa Maneno Yake (A.S)

Miongono mwa maneno yake (a.s)- Hotuba hii Al'Barqii ameielzea katika kitabu "Al'Mahasin" katika kitabu cha 'Masabiihu dhulmi'. Na at-Tawhidii ndani ya "Al'Basairu wa Dhakhairu" uk. 32. Na ibn Waadhihu ndani ya "At-Tari'ikh": Jz. 2, uk. 136. Na Al'Kaulayni ndani ya "Al'Kaafii" katika mlango wa Al'bid'au war'ra'ayu

Kuhusu chanzo cha fitna:

"Hakika chanzo cha kutokea fitina ni kuendekeza na kufuata matamanio, na hukumu huzushwa, humo

Kitabu cha Mungu huendwa kinyume, kwa hilo watu wanasaidiana wao kwa wao[1]kinyume na dini ya Mungu. Lau batili ingekuwa tupu bila ya kuchanganyika na haki isingefichika kwa wenye kuitafuta; Na lau haki ingekuwa imeepukana na kuvikwa na batili, ndimi za wapinzani zingekatika.

Lakini huchukuliwa kutoka huku fumba[2] na huku fumba na huchanganywa, hapo shetani huwashinda rafiki zake, wataokoka wale waliotunukiwa wema kutoka kwa Mungu hapo kabla."

---

1. Watu wanasaidiana. Anasema (a.s): Kwa kweli madhehebu za batili na rai mbovu ambazo kwazo watu wanakumbwa na fitna, asili yake ni kuifuata hawaa – matamanio ya nafsi, na kuzua hukumu ambazo hazikujulikana (na dini) zilizo kinyume na Kitabu, ushabiki na matamanio ya nafsi humchukua mtu kuwapenda watu wayasemayo hayo (ya bid'a), bila ya uthibitisho kutoka (dalili za) dini. Nguzo ya kutokea kwa mkanganyiko huu wote ni kule kuchanganyika kwa haki na batili katika maoni.
2. Fumba: (fumba hapa ni tafsiri ya: yaani ujazo mmoja wa kicha cha majani yaliyochanganyika kati ya mabichi na makavu, Mungu (swt) amesema: "Na shika kicha cha majani mkononi mwako, kisha ndio upigie nacho" (Surat Swad: 44). Anamaanisha (a.s) kuwa ikitendwa haki kama ilivyo haitoshabihiana na batili, iangaliwapo batili hujitokeza kana kwamba kuna sura ya haki kwa hiyo anakanganyikiwa, hiyo ndiyo fumba la haki na hiyo ni: fumba la batili. Na machimbuko ya matamanio ya kinafsi ndio chanzo cha kutokea kwa fitna, na hiyo ni kutokana na kuchanganyika kati ya haki na batili.

51. Na Miongoni Mwa Khutba Zake (A.S)

Na miongoni mwa khutba zake (a.s) – Ameieleza hotuba hii ibn Muzahim ndani ya kitabu chake,'*Swifiin*.'

Watu wa Muawiyah walipowazidi nguvu watu wake (a.s) kwa kuzingira njia ya maji na kuwaziwia wasiteke maji kutoka mto wa Furati huko Siffin:

"Wamekuombeni vita, basi bakieni katika madhila na kubaki nyuma kwa daraja, au zikozeni kiu panga kwa damu mtakoza kiu zenu kwa maji: Mauti hasa ni maisha ya kuburuzwa, na uhai hasa ni kufa ndani ya kutenzwa nguvu. Lo! kwa hakika Muawiyah ameongoza kikundi cha watu waasi na amewafichia kheri kiasi cha kuwa wamezifanya shingo zao ziwe shabahio la mauti."

52. Miongoni Mwa Khutba Zake (A.S)

Miongoni mwa khutba zake (a.s) – Hotuba hii inaifuata hotuba iliyotangulia katika nakala ya ibn Abil–Hadid.

Kuhusu kujinyima:

“Lo! Kwa kweli dunia imekwisha na imetoa ilani kwisha kwake. Mema yake, yameondoka yametokomea haraka, inawasukumia mwisho wakazi wake, inawasukuma kwenye umauti majirani zake. Vilivyokuwa vitamu imevifanya kuwa vichungu, na kuvichafua vilivyo kuwa safi, hakikubakia humo ila mabaki kidogo kama mabaki ya maji katika chombo au mfano wa funda la mgao, lau wenye kiu wawili wafyonze hawangekata kiu.

asi enyi waja wa Mungu azimieni msafara wa kuitoka nyumba hii ambayo wakazi wake wamepangiwa kutoweka, wala yasikushindeni nguvu humo matumaini, wala muda msiufanye kuwa mrefu humo. Wallahi hata mlie mfano wa ngamia walio huzunika kwa kuwakosa watoto wao au muite kwa mnung’uniko wa huzuni wa njiwa, au mnyanyue sauti kwa unyenyekevu mfano wa watawa (waliojitenga na dunia wakimuelekea Mungu,) na muwe mmejitowa mbali na mali na watoto mkimuelekea Mungu; kutaka ukaribu na yeye, ili kuinyanyua daraja kwake au kughufiriwa ovu lililohesabika na vitabu Vyake, na kuhifadhiwa na malaika Wake, ingekuwa thawabu kidogo kulinganisha na ninavyowatarajia thawabu Zake, na ninavyo wahofia adhabu Zake.

Namuapa Mungu hata nyoyo zenu ziyayuke kabisa na macho yenu yatiririshe machozi ya damu aidha mkimtarajia au kumhofia, kisha mbakishwe kuishi duniani muda wake wa kudumu, matendo yenu hayangetoa malipo ya neema Zake kubwa – hata kama msingebakisha kitu katika juhudi zenu – zisingelipia chochote katika fadhila Zake nyingi juu yenu – na kuwaongozeni kwake kwenye imani.”

53. Na Miongoni Mwa Khutba Zake (A.S)

Katika kuielezea siku ya kuchinja na hali ya mnyama atakiwaye kuchinjwa:

“Na miongoni mwa ukamilifu wa mnyama achinjwaye ni kunyooka na kuinuka masikio yake na usalama wa macho yake. Endapo masikio na macho yatakuwa salama, mnyama wa kuchinjwa atakuwa amekamilika na ametimia. Japo awe mweye kuvunjika pembe na yu auvuta mguu wake kwenda machinjioni”.[1]

Sayyid Ar–Radhiy amesema*: “*Na *mansaku* hapa ni mahali pa kuchinjia.”

---

1. Anakokota mguu wake akielekea kwenye machinjio: Maana yake ni kinaya cha aliyelemaa mguu (kiguru). Na katika sifa za mnyama wa kuchinjwa na aibu zake, kuna maelezo na tofauti nyingi ndani ya vitabu vya fiqhi.

54. Na Miongoni Mwa Khutba Zake (A.S)

Na miongoni mwa khutba zake (a.s) – Ameitaja hii Ibn al–Athir katika kitabu an–Nihaya kwenye mada ya Dakaka, jalada la pili, uk. 128. Rejea mwanzo wa hotuba ya 26.

Pindi waliposongamana watu ili kumfanyia bai'a:

"Walisongamana kwangu msongamano wa ngamia wenye kiu, siku ya kunyweshwa kwao, pale mchunga wao akiwa amewapeleka, na wameondolewa kamba; ilifika hali nidhanie wataniua, au baadhi yao watawauwa baadhi mbele yangu. Na nimeliangalia jambo hili kwa kuligeuza nje ndani kiasi cha kunizuia usingizi, sikuwa na njia ila kupigana nao, au kuyakanusha aliyoyaleta Muhammad (s.a.w): Nikaona kuikabili vita1 ni wepesi kwangu kuliko kuikabili adhabu, na mauti ya dunia ni mepesi kwangu kuliko mauti ya akhera."

---

1. Kuwapiga vita madhalimu ni wajibu juu ya imam pindi akiwa na wasaidizi, akiacha kufanya hivyo atakuwa amewacha kutekeleza wajibu, kwa hilo atakuwa anastahiki adhabu, na atakuwa mwenye kuitelekeza amri ya Mungu kwa kuacha alilomuwajibishia, anakuwa mwenye kupinga aliyokuja nayo Mtume wa Mungu (s.a.w.w.).

55. Miongoni Mwa Maneno Yake (A.S)

Swahaba zake waliona kwamba ameichelewesha idhini ya kupigana huko Siffiin:

"Ama kauli yenu kuwa: 'yote haya yanatokana na kuuchukia umauti?' Namuapa Mungu sijali iwe nimeingia kwenye umauti au umauti umenijia.1

Ama kauli yenu kuwa amekuwa na shaka ya kuwapiga watu wa Shamu! Wallahi sikuacha vita hata siku moja ila nikiwa na matumaini kuwa kundi la watu likutane na mimi na liongoke na mimi, liangaze kwa mwanga wangu japo kwa mtazamo finyu2 na hilo lanipendeza mno kuliko niliuwe (kundi la watu) hali likiwa ndani ya upotovu; japokuwa linarejea na dhambi zake.

---

1. Watu wake waliona amechelewesha idhini yake kuwapiga watu wa Sham (Syria). Walihitilafiana kuhusu sababu ya kuchelewa. Baadhi yao walisema: "ni kwa sababu ya kuchukia mauti." Na baadhi yao wakasema: "Ni shaka ya kuwa je! Yafaa kuwapiga watu wa Sham!" Hapo akawajibu: "Kuhusu mauti hakuwa wa kuyaogopa, na kuhusu shaka haina nafasi, isipokuwa anataraji kwa kuzuia vita wapate kuiepuka na wamjie bila ya vita, kwani hilo lampedeza mno kuliko kupigana hali watu wakiwa ndani ya upotovu, japo iwe dhambi ni yao."

2. Amewashabihisha na ambao huenda wangejiunga na yeye miongoni mwa watu wa Sham na ambaye anabubusa usiku kuuelekea moto; na hivyo ni kwa sababu macho yao ni dhaifu, hivyo wao kuongoka na mwongozo wake (a.s.) ni kama anayebubusa kwa udhaifu wa macho yake kuuelekea moto wakati wa usiku. Alisema: Hilo ni bora kwangu kuliko niwauwe wakiwa katika upotofu, ingawa endapo nitawaua nao wakiwa katika hali hii watarejea na dhambi zao. Yaani, watakuwa wamerejea, amesema swt: “Mimi ninataka urejee na dhambi zangu na zako!” al-Maida: 29

Orodha Ya Vitabu Vilivyo Chapishwa Na Al-Itrah Foundation:

1. Qur'an Al-Kariim – Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Ishirini.
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abu Dharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'ani na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shi’ah
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'ani Tukufu
27. Al-Wahda

28. Ponyo kutoka katika Qur'ani.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyeezi Mungu na sifa zake
36. Amateka na Aba'Khalifa
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana.
39 Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Nyuma yaho naje kuyoboka
41. Amavu n'amavuko by'ubushiya
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shi'ah
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'ani inatoa changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Minan-Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mitume Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu

67. Tujifunze Misingi Ya Dini
68. Sala ni Nguzo ya Dini
69. Mikesha Ya Peshawar
70. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
71. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliy onyooka
72. Shi'ah asema haya, Sunni asema haya, Wewe wasemaje?
73. Liqaa-u-llaah
74. Muhammad (s.a.w.w.) Mtume wa Allah
75. Amani na Jihadi Katika Uislamu
76. Uislamu Ulienea Vipi?
77. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s.a.w.w.)
78. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s.a.w.w.)

Back Cover

NAHJU 'L-BALAGHAH ni jina la majimui (mtungo) maarufu ya khutba, amri, barua, risala, mawaidha na semi fasihi za Imam Ali bin Abu Talib (a.s.). Haya yote yamekusanywa na Abu 'l-Hasan Muhammad bin Husain al-Sharif al-Radhii.

Mtungo huu wenye khutba takriban 237, amri (hukumu), barua na risala 79, na semi (methali) 480 ulikamilika mwezi wa Rajab 400 A.H./1009 A.D. Maana ya *nahj* ni 'njia iliyo wazi' au 'barabara kuu'; na maana ya *balaghah* ni ufasaha wa lugha (balagha); elimu ya usemaji mzuri na safi wa lugha, n.k. Kwa hivyo, *Nahju 'l-Balaghah* maana yake ni Barabara Kuu ya Ufasaha.

"Mtu yeyote ambaye amebobea katika lugha ya Kiarabu atakubali tu kwamba baada ya maneno matukufu ya Mwenyezi Mungu na Mtume Wake Muhammad (s.a.w.), *Nahju 'l-Balaghah* inafuata kwa ubora wake. Maneno ya Ali ni yenye maana na fikra nzito..." (Sheikh Abbas Mahmud al-'Aqqad - mwandishi mashuhuri wa Kimisri)

"Ali alikuwa ni Imamu (kiongozi) kwenye nyanja za vita, Imamu wa siasa, Imamu wa dini, Imamu wa falsafa, Imamu wa maadili, Imamu wa maandiko mbalimbali, na Imam wa elimu na hekima."
('Abdu 'l-Masih al- 'Antaqi - Mhariri wa Kikristo wa gazeti la Kimisri la *al-Ahraam*)

"Mtu yeyote anayetamani kuikata kiu yake (ya kiroho) kwa maneno ya Ali (a.s.), lazima ausome kila ukurasa wa *Nahju 'l-Balaghah*." (Amin Nakhlah)

Kimetolewa na kuchapishwa na:
Alitrah Foundation
S.L.P. 19701 Dar es Salaam, Tanzania
Simu: 255 22 2110640 / 2127555
Barua Pepe: alitrah@raha.com [14]

Tovuti: www.ibn-tv.com

Source URL: https://www.al-islam.org/node/24794

Links

[1] https://www.al-islam.org/user/login?destination=node/24794%23comment-form

[2] https://www.al-islam.org/user/register?destination=node/24794%23comment-form

[3] https://www.al-islam.org/organization/al-itrah-foundation-0

[4] https://www.al-islam.org/person/shaikh-harun-pingili

[5] https://www.al-islam.org/person/ustadh-abdul-karim-nkusui

[6] https://www.al-islam.org/person/dr-ja%E2%80%99far-atijani

[7] https://www.al-islam.org/person/ramadhani-kanju-shemahimbo

[8] https://www.al-islam.org/library/imam-ali

[9] https://www.al-islam.org/tags/khutba

[10] https://www.al-islam.org/tags/barua

[11] https://www.al-islam.org/tags/risala

[12] https://www.al-islam.org/person/imam-ali-1

[13] https://www.al-islam.org/person/mtume-muhammad-saw

[14] mailto:alitrah@raha.com